# Nipashe

Ijumaa Juni 5, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580250

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## Ewura: Msihifadhi petroli ndani mnajitengenezea bomu

UK. 3




UKURASA 11

# Kinana amwangukia JPM


UKURASA 2

## BAA LA CORONA



Uwezekano wa washiriki na washangiliaji kutoka nje wanaotumia usafiri wa umma kupata maambukizo ya Covid-19 sio mkubwa ikilinganishwa na wale wa ndani wanaotumia usafiri huo kila siku bila kuzingatia ukaaji wa kuachiana nafasi. WHO.

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Dk. John Magufuli, akiteja jambo na Katibu Mkuu mstaafu wa chama hicho, Abdulrahman Kinana, katika moja ya shughuli za chama hicho. **PICHA: MAKTABA**.





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play | Download on the App Store


## Waziri afunguka zuio la mikutano

- Ni ya vyama kujiandaa kuelekea Oktoba... *Uk. 2*

## WAZIRI ASHANGAA SUKARI KUPOTEA

UKURASA 3


**MICHEZO** MAMBO MATAMU YASUBIRIWA YANGA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Waziri Simbachawene afunguka zuio mikutano

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema hana maelekezo ya kuzuia mikutano ya vyama vya siasa kuelekea Uchaguzi Mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana katika mahojiano maalum kuhusu mikutano ya vyama vya siasa kama inaruhusiwa kufanyika au la kuelekea Uchaguzi Mkuu, Waziri Simbachawene alisema: "Sina maelekezo ya kuzuia mikutano ya vyama vya siasa kwa sababu sijawahi kupewa hicho kitu.

"Bali, Jeshi la Polisi linaweza kutoa kibali cha mikutano pale ambapo hakuna hofu ya uvunjifu wa amani, kama ipo basi linaweza lisitoe likaelekeza vinginevyo."

Alisema hilo linathibitiwa na sheria nyingine, lakini wao kazi yao ni kutoa vibali kwa mtu anayeona anataka kufanya shughuli yoyote ya mikusanyiko ya watu.

"Ukitaka kufanya shughuli yoyote ya mikusanyiko ya watu kama injili, chama cha siasa au wafugaji wa ng'ombe au walina asali, sisi kazi yetu ni kutoa kibali pale tunapohisi kuna tishio la uvunjifu wa amani linaloweza kutokea kutokana na jambo hilo tunaweza kuzuia na kuelekeza vinginevyo.

Alipoulizwa kuhusu vibali ambavyo vimeshatolewa hadi jana kwa ajili ya mikutano ya vyama vya siasa, Waziri Simbachawene alisema hivi karibuni hawajapata maombi yoyote.

"Wapeleke maombi ya kufanya mikutano Jeshi la Polisi na jeshi litaangalia kama wanaruhusiwa kufanya kwa maana hakuna tishio lolote la uvunjifu wa amani wanaweza kuruhusiwa," alisema.

Kuhusu Jeshi la Polisi lilivyojiandaa kwenye ulinzi na usalama wakati wa uchaguzi, alisema wamekuwa wakifanya hivyo siyo tu kwenye uchaguzi.

"Wakati wote tumekuwa tukihakikisha ulinzi na usalama unaokuwapo, tunahakikisha shughuli zote za maendeleo zinafanyika bila shida, ikiwamo uchaguzi.

"Nikisemea uchaguzi peke yake ni kama ni jambo mahsusi sana katika muhktadha mzima wa amani na utulivu katika nchi, niseme tu kwamba Jeshi la Polisi wakati wote tupo imara kuhakikisha nchi ipo salama ndani ya mipaka na wananchi wanaendelea kufanya shughuli zao."

Hata hivyo, alisema kuelekea uchaguzi mkuu, wananchi wawe watulivu kwa sababu Jeshi la Polisi limejipanga vizuri kuhakikisha unafanyika salama.

Baada ya kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, serikali ilizuia mikutano ya kisiasa, isipokuwa kwa madiwani na wabunge ambao waliruhusiwa kufanya hivyo katika maeneo yao.

Hata hivyo, vyama vya siasa hivi karibuni vimeanza kulalamikia kuendelea kuwapo zuio hilo wakati umebaki muda mfupi wa kwa maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akimshika mmoja wa ng'ombe waliokuwa katika josho la kuogeshea mifugo, katika Kijiji cha Mwakisandu, wilayani Meatu, mkoani Simiyu juzi, ambapo alikagua ukarabati na ujenzi wa josho la kuoshea mifugo la Kijiji cha Mwakisandu na Isangijo. Habari Uk. 9. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**.

# Kinana amwangukia JPM

**Na Asraji Mvungi, ARUSHA**

ALIYEKUWA Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Abdulrahaman Kinana, amemwomba msamaha hadharani Mwenyekiti wa CCM, Taifa, Dk. John Magufuli.

Kiongozi huyo ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa CCM wakati wa Serikali ya Awamu ya Nne, alitangaza hadharani kuomba msamaha huo kwa makosa aliyoyatenda kipindi chake cha uongozi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha jana, Kinana alisema akiwa kiongozi anaamini kuwa yapo mambo aliyoyafanya ambayo yaliwakwaza viongozi wengine akiwamo Mwenyekiti wa CCM, Dk. John Magufuli, ambaye ni Rais wa Tanzania na anaamini atamsamehe.

"Naamini ilifika wakati nikakereka na kusema maneno ambayo yanaweza kuwa siyo mazuri, nimekaa na kutafakari sasa, namuomba radhi Mwenyekiti wa CCM, Magufuli," alisema Kinana na kuongeza:

"Kama kiongozi ni kweli naamini ilifikia hatua nikatofautiana na wenzangu ama niliwakera wenzangu na pia, hata kiongozi wangu, Mwenyekiti wa Chama, kiukweli ninamwomba radhi."

Akiwa Arusha, Kinana pia alikutana na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Zelote Steven na Katibu wa Mkoa wa huo, Mussa Matoroka na kuwaeleza kuwa pamoja na kustaafu, ataendelea kutoa ushirikiano wa hali na mali ndani na nje ya chama chake.

> **Mimi kwa sasa nimestaafu uongozi, ninamshukuru Mungu na ninaendelea kujifunza, kusoma vitabu na kufanya mazoezi na niko tayari kuendelea kutoa mchango wangu wa hali na mali ndani na nje ya chama**

"Mimi kwa sasa nimestaafu uongozi, ninamshukuru Mungu na ninaendelea kujifunza, kusoma vitabu na kufanya mazoezi na niko tayari kuendelea kutoa mchango wangu wa hali na mali ndani na nje ya chama," alisema.

Akizungumzia hatua hiyo, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Steven, alimpongeza Kinana kwa uamuzi huo na kwa moyo wa kuendelea kutoa mchango kwa chama ikiwamo kuwasaidia wanasiasa wachanga.

Desemba 13, mwaka jana, Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM (NEC), iliagiza makada watatu wa chama hicho akiwamo Kinana, waitwe na wahojiwe na Kamati ya Maadili na Usalama, baada ya kutuhumiwa kwa makosa ya kufanya mambo kinyume na taratibu za chama.

Kamati Kuu, iliwaadhibu viongozi hao na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, kufukuzwa uanachama kwa kukiuka maadili ya chama hicho.

Kadhalika, Makamba alisamehewa huku Kinana akipewa barua ya onyo ikiwamo kuwa chini ya uangalizi kwa miezi 18 na kuzuiliwa kujihusisha kugombea nafasi yoyote ndani ya chama hicho.

Kinana na aliyekuwa Katibu Mkuu wa miaka mitano ya kwanza ya serikali ya awamu ya nne, Yusuph Makamba, waliibua mjadala mkali baada ya sauti zao kuvuja mitandaoni wakizungumzia mpasuko ndani ya chama hicho.

Julai 14, mwaka jana Kinana na Makamba waliwasilisha malalamiko yao wakidai kuwa uongozi wa chama hicho hauwalindi dhidi ya mtu aliyekuwa akiwadhalilisha kwenye mitandao ya kijamii.

Walikuwa wakilalamikia kuchafuliwa na kudhalilishwa na mtu anayejiita mwanaharakati na mtetezi wa serikali ya Rais John Magufuli.

Siku chache baadaye zilisambaa sauti zinazodaiwa ni mazungumzo kwa njia ya simu baina ya Makamba na Kinana.

Kinana na Makamba walifikisha waraka wao kwa Katibu wa Baraza la Ushauri la Viongozi Wakuu Wastaafu, Pius Msekwa.

Kwa upande wake Kanali Mstaafu Kinana alipokea wadhifa wa Katibu Mkuu mwaka 2012 hadi 2018 kutoka kwa Wilson Mukama aliyeshikilia wadhifa huo kati ya mwaka 2011-2012.

## HABARI KITAIFA

# Mpigapicha wa Waziri Mkuu azikwa




Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Tom Apson, akiweka udongo kwenye kaburi la aliyekuwa mpigapicha wa Waziri Mkuu, Christopher Mfinanga, wakati wa mazishi yaliyofanyika katika makaburi ya familia katika kijiji cha Mangio, Vuchama, wilayani Mwanga, mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: OWM.**

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Mwanga, Tom Apson, ameongoza mazishi ya aliyekuwa Mpigapicha wa Waziri Mkuu, Chris Mfinanga, yaliyofanyika kwenya kijiji cha Mangio, Vuchama, wilayani humo.

Akizungumza na waombolezaji kijijini hapo jana, Mkuu huyo wa Wilaya ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mgwira, alisema Mfinanga alikuwa mtu aliyejaa upendo ndiyo maana wengi wanahuzunishwa na kifo chake.

"Chris alikuwa mtu mcheshi na mwenye upendo, alisaidia wengi, lakini tusisahau Mungu ndiye mtoa riziki. Msikate tamaa kwa sababu Mungu yupo na alimwezesha Chris na ndiyo maana aliweza kuwasaidia wengine na hata kuwasomesha watoto wenu."

"Ninawasihi muamini kuwa Yesu yupo na kwake kuna faraja. Amini Yesu yupo na usiamini katika mganga wa kienyeji au ushirikina. Tuache ramli, tumtegemee Mungu nasi tutapata faraja," alisisitiza.

Akiongoza ibada hiyo, Mchungaji Kiongozi wa KKKT Usharika wa Vuchama, Bill Graham Msangi, aliwataka waombolezaji waweke mambo yao sawa na Mungu wao pamoja na majirani wanaoishi nao.

Akitoa mahubiri kutoka kitabu cha Ufunuo wa Yohana (14:13), Mchungaji Msangi alisema watu wanaomwamini Kristo wana heri kwa sababu wanapoaga dunia ni sawa na watu wanaoenda kupumzika baada ya taabu zao hapa duniani. "Wanaokufa katika Bwana wanaenda kupumzika baada ya taabu zao. Wana heri sababu matendo yao yanafuatana nao."

"Neno la Mungu limesema; bali wao wasioamini, waongo wote, wachukiao na wezi wote na waabuduo sanamu, sehemu yao ni kwenye ziwa la moto ambao hata mende hawaungui. Hata uwe tajiri kiasi gani, au uwe mzuri kiasi gani au uwe baunsa, hautaweza kuzuia kuingia kwenye jehanamu ya moto eti kwa sababu ya ubaunsa wako."

"Tunapaswa tujiandae kwa sababu siku ikifika, Mungu hataangalia uzuri ulionao. Yeye Mungu ni mzuri kuliko huo uzuri wako. Shetani alikuwa mzuri sana, lakini alipoasi alifukuzwa."

Aliwasihi wafiwa na wakazi wa kijiji hicho hao wawe na umoja ili amani iweze kutawala. "Umoja ukae miongoni mwa familia, ukae miongoni mwa kaya nyingine na wanavijiji wote. Tukiishi kwa namna hiyo, amani itatawala kwa sehemu kubwa."

Naye Padre Japhet Njaule wa Parokia ya Vuchama ambaye aliongoza mazishi ya baba yake Chris Mei 21, 2020, aliwataka waombolezaji wamtumaini Mungu na waishi kwa kujiandaa na kuwa tayari wakati wote.

# Ewura: Msihifadhi petroli ndani mnajitengenezea bomu

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nishati, Maji na Mafuta (Ewura), imewaonya wafanyabiashara wa mafuta na wananchi kutohifadhi mafuta katika kipindi hiki yaliposhuka bei kwa kuwa wanajitengenezea bomu linaloweza kulipuka wakati wowote.

Akizungumza na Nipashe, Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa Ewura, Titus Kaguo, alisema kuhifadhi mafuta ndani ni sawa na kuishi na bomu ambalo litalipuka wakati wowote, na ndiyo maana huchimbiwa ardhini.

Vile vile, alisema wafanyabiashara wa mafuta wasithubutu kuhifadhi ili walangue wananchi baadaye, na kwamba wakifanya hivyo Ewura inajua.

"Tunawaonya wafanyabiashara wenye maghala na kwa makusudi wakashindwa kuuza mafuta kwa lengo la kuyaficha wajue ni hatari kubwa inakuja kwao," alisema na kuongeza:

"Mifumo ya Ewura tunajua kiasi cha lita tulizonazo na jinsi inavyotumika kila siku, tunajua wanaoweza kuhifadhi ni wale wauzaji wa jumla na tunawafuatilia kila wakati."

Alisema Ewura inajua kuwa wenye uwezo wa kuhifadhi ni wauzaji wakubwa na iwapo itagundulika watachukuliwa hatua kali za kisheria, huku akibainisha wapo walioandikiwa barua ya onyo kwa makosa mengine.

"Tunafuatilia kwa karibu ukiukaji wa bei za mafuta, mtiririko wa uuzaji wa mafuta kwa kuwa tuna mifumo thabiti ya kutambua kila udanganyifu," alisema.

Juzi, Ewura ilitangaza kushuka bei ya mafuta hayo na jijini Dar es Salaam bei ya rejareja ya petroli ni Sh. 1,520, dizeli Sh. 1,546 huku mafuta ya taa yakiuzwa Sh. 1,568.

Mkoani Arusha, bei ya rejareja ya petroli ni Sh. 1,711, dizeli Sh. 1,750 na mafuta ya taa Sh. 2,044, huku Dodoma petroli ikiuzwa kwa Sh. 1,579, dizeli 1,605 na mafuta ya taa Sh. 1,627.

Mkoani Kilimanjaro petroli ni Sh. 1,700, dizeli Sh. 1,739 na mafuta ya taa ni Sh. 2,033, Mbeya mafuta petroli Sh. 1,627, dizeli Sh. 1,653 na mafuta ya taa ni Sh. 1,675 na Geita petroli Sh. 1,685, dizeli Sh. 1,712 na mafuta ya taa Sh. 1,733.

# Waziri ashangaa kupotea kwa sukari

**Na Mary Geofrey**

WAKATI sukari ikiendelea kuwa bidhaa adimu katika baadhi ya maeneo mbalimbali nchini, serikali imesema haifahamu inapofichwa kwa sababu ipo ya kutosha.

Imesema kwa sababu ya sintofahamu hiyo, wameandaa mpango mkakati wa kuanza kusaka inapofichwa sukari hiyo kuanzia Jumatatu ya wiki ijayo.

Waziri wa Kilimo, Japhet Asunga, aliyaeleza hayo jana, wakati akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu na kusema kuwa, kinachofanyika ni uhuni kwa sababu bidhaa hiyo ipo kwa wingi nchini.

"Kinachofanyika ni uhuni, kwa sababu sukari ipo ya kutosha, hatuna uhaba wa sukari nchini," alisema Asunga.

Alieleza kuwa, kwenye maduka ya jumla hakuna uhaba wa sukari na inauzwa kwa bei elekezi, hali inayoifanya serikali kushindwa kufahamu sababu ya bidhaa hiyo kutowafikia wananchi, lakini kutokuuzwa kwa bei elekezi.

"Hatujui kwa nini sukari iuzwe bei ya juu, wakati ipo ya kutosha, tutapita duka kwa duka kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa kubaini wale wote wanaoleta fujo kwenye bidhaa hii," alisema Asunga.

Alisema kwa kuanza wataanza na mkoa wa Dar es Salaam, ambako kuna bandari inayoshusha bidhaa hiyo hivyo hakukuwa na sababu yoyote ya kuwa adimu.

Asunga alisisitiza kuwa, watapita katika maduka na maeneo ambako wanadhani kuwa bidhaa hiyo imefichwa na watafika katika mikoa yote nchini.

HALI ILIVYO DAR

Nipashe jana lilipita katika baadhi ya maduka katika jijini la Dar es Salaam zikiwamo 'Super market' na kukuta bidhaa hiyo ikiuzwa kwa mashati na wengine wakiuza kwa bei ya kati ya Sh. 3,000 na 4,000.

Katika duka kubwa la Mlimani City jana kilo moja ya sukari ilikuwa ikiuzwa kwa bei elekezi ya Sh. 2,600, lakini kwa masharti ya kila mteja kununua kilo mbili peke yake.

"Nimeenda kununua sukari pale Mlimani City kwa masharti ya kutochukua zaidi ya kilo mbili na wakati natoka ndani pale ikawa ishamalizika kwa hiyo wateja waliongia nyuma yangu walikosa," alisema mmoja wa wanunuzi wa sukari.

Katika maeneo ya Mwananyamala, sukari inapatikana katika baadhi ya maduka na kwa bei ya kuanzia Sh. 3,500 hadi 4,000 kulingana na matakwa ya muuzaji.

"Unakuta duka hili linauza Sh. 3,600, lingine 3,700 na mengine yanauza 4,000 lakini siyo maduka yote ni baadhi tu ambayo yanauza," alisema Jumanne Khamis mkazi wa Mwananyamala.

Katika maeneo ya Tabata Segerea, sukari inauzwa katika baadhi ya maduka kwa bei ya Sh. 3,500 na maduka mengine wanauza ikiwa imeshapimwa na kufungwa kwenye vifungashio.

Katika maeneo ya Kimara sukari inauzwa Sh. 3,500 katika baadhi ya maduka, wakati maduka mengine yakiwa hayana bidhaa hiyo.

Nipashe lilipita katika baadhi ya maduka ya jumla na kukuta sukari ikiuzwa kati ya Sh.125,000 na 128,000 kwa kilo 50 kutoka Sh. 140,000 hadi 150,000 kwa siku za nyuma.

Itakumbukwa kuwa, Mei 14, mwaka huu, Waziri wa Viwada na Biashara, Innocent Bashungwa, alipokea shehena ya tani 600 ya sukari katika bandari ya Mwanza ikitokea nchini Uganda.

# Umoja wavitesa vyama vya upinzani

**Na Romana Mallya**

SIKU chache baada ya vyama vya Chadema na NCCR-Mageuzi, kutangaza kufungua milango kwa vyama vingine vya upinzani vilivyotayari kushirikiana kuikabili CCM , ACT-Wazalendo imefunguka.

Juzi Chadema ilitangaza kufungua milango kwa vyama vya upinzani kushirikiana navyo kuing'oa CCM, na jana NCCR -Mageuzi ilitangaza jambo hilo hilo.

Kutokana na hali hiyo, Nipashe iliviuliza vyama ambavyo havijazungumzia ushirikiano huo, na ACT-Wazalendo kilisema nia na dhamira yake ya siku nyingi ya kushirikiana na vyama vingine kueleka Oktoba iko pale pale.

Naibu Katibu wa Uendezi Habari na Mahusiano kwa Umma wa chama hicho, Janeth Rithe, akizungumza na Nipashe alisema kwa muda mrefu chama hicho kilizungumzia ushirikiano huo na wapo tayari kushirikiana na chama chochote.

"Mdau mkubwa wa kwanza ambaye anataka ushirikiano na vyama vingine vya siasa vya upinzani ni ACT-Wazalendo, tulishaanzisha mazungumzo na vyama mbalimbali, ili tushirikiane kwenye uchaguzi na kwenye kutoa misimamo ya vyama," alisema.

Alisema hivi sasa bila ya kuwa na umoja na kuzungumza na kutoka na kauli moja kunakuwa na mgawanyiko.

**CUF: TUNASUBIRI VIKAO**

Naye, Naibu Katibu Mkuu Bara wa Chama cha Wananchi (CUF), Magdalena Sakaya, alisema mambo yao mengi huamuliwa kwenye vikao ambavyo vinatarajia kuanza mwishoni mwa wiki ijayo.

"Maandalizi yetu ya uchaguzi na mambo mengine yanayojitokeza kama kuna umuhimu au hakuna umuhimu yatategemea na vikao vya maamuzi ambavyo vitaanza mwishoni mwa wiki ijayo, tutashauriana kuona kama kuna ulazima au hakuna ulazima," alisema.



Wafanyakazi wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), wakiwa katika chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kughushi, kula njama, kuisababishia serikali hasara na kutakatisha Sh. milioni 18.5. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

# Vigogo 4 Nemc washtakiwa uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

VIGOGO wanne wa Baraza la Usimamizi wa Mazingira (Nemc), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kughushi, kula njama, kusaababishia serikali hasara na kutakatisha Sh. milioni 18.5.

Washtakiwa hao wamesomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali, Janeth Magoha, akisaidiana na Waendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Stanley Lugola na Sofia Nyanda.

Magoha aliwataja washtakiwa hao kuwa ni, Deusdedith Katwale, Magori Matiku, Obadia Machupa na Mhasibu Msaidizi wa Nemc, Lydia Nyinondi.

Upande wa Jamhuri ulidai, katika shtaka la kwanza washtakiwa wote wanadaiwa kati ya Juni mosi, 2016 na Julai 30, 2017 ndani ya Jiji la Dar es Salaam na Dodoma, walikula njama ya kutenda makosa ya kughushi, kutoa nyaraka iliyoghushiwa, kuisababishia mamlaka hasara na kutakatisha fedha.

Katika mashtaka ya kughushi imedaiwa, kati ya Agosti mosi, 2016 na Septemba 6, 2017 huko Kinondoni, jijini Dar es Salaam na mkoani Dodoma, mshtakiwa Katwale alighushi ripoti ya kutathmini mazingira ya mradi wa kituo cha mafuta cha Ibra General Enterprises, kitalu namba 132, Block T Chadulu Area A, Dodoma kwa dhumuni la kuonyesha kwamba tathmini ya mazingira ya mradi huo ilikuwa imefanyika huku akijua kuwa siyo kweli.

Pia, mshtakiwa huyo anadaiwa kughushi kikao cha tathmini ambayo ni nyaraka ya 'Minutes for Technical Advisory Committee (TAC)' kuonyesha kwamba kikao hicho kilichofanyika huku mshtakiwa Lydia akidaiwa kuwa Julai 5, 2016, maeneo ya Ofisi za Nemc Kinondoni, alighushi risiti yenye thamani ya Sh. milioni 18.5 kuonyesha kuwa zimelipwa kwa NEMC.

Katika shtaka la tano, imedaiwa kuwa, kati ya Juni mosi, 2016 na Julai 30, 2017 katika Ofisi za Nemc Kinondoni, mshtakiwa Katwale aliwasilisha nyaraka ya uongo kwa Mkurugenzi wa Nemc kuhusu mradi wa mafuta wa Ibra General Enterprises, kuonyesha kuwa ukaguzi wa mradi huo ulifanyika huku akijua kuwa siyo kweli.

Luoga, alidai kuwa Julai 5, 2016, Matiku aliwasilisha nyaraka ya uongo akionyesha risiti kwa Yunis Mfala.

Uliendelea kudai kuwa, washtakiwa hao pia wakiwa watumishi wa Nemc walikiuka kifungu cha 29 cha Sheria ya Usimamizi Mazingira, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 na hivyo, kujipatia Sh. milioni 18.5 kwa ajili yao.

Katika mashtaka ya kusababisha hasara, imedaiwa kati ya Juni mosi, 2016 na Julai 30, 2017 huko Kinondoni, washtakiwa hao kwa pamoja wakiwa watumishi wa Nemc na nia ovu waliisababishia mamlaka hiyo hasara ya Sh. milioni 18.5.

Katika shtaka la tisa la utakatishaji, imedaiwa siku na mahali hapo washtakiwa hao walijipatia kiasi hicho cha fedha toka kwa Mfala ambaye ni mmiliki wa mradi wa kituo cha mafuta cha Ibra General Enterprises, huku wakijua kuwa fedha hizo ni zao la kosa tangulizi la kughushi.

Washtakiwa wamekana mashtaka hayo.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) ametoa kibali cha kuendelea kusikiliza kesi hiyo.

Wakili wa utetezi, Dk. Rugemeleza Nshala, aliomba dhamana kwa wateja wao kwa sababu Mahakama Kuu imeshatoa uamuzi kwamba mashtaka ya utakatishaji fedha yanadhaminika.

Hata hivyo, Luoga alipinga hoja hiyo kuwa mashtaka ya utakatishaji fedha hayafahamiki na wanafahamu uwapo wa kesi ya kikatiba ambayo iliamriwa na Mahakama Kuu na kuongeza kuwa, mahakama iliwapa muda wa miezi 18 serikali kufanya mabadiliko ya sheria iliyozuia dhamana kwa washtakiwa wa makosa ya utakatishaji fedha yadhaminike na kabla ya hapo sheria iendelee kutumika kama kawaida.

Hata hivyo, Dk. Nshala alidai mahakama inayo mamlaka ya kutoa amri yoyote kuhusu dhamana ambayo ni haki ya kikatiba ya washtakiwa.

# Wasimamishwa kazi Maliasili kupisha uchunguzi bil. 4/-

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WIZARA ya Maliasili na Utalii imewasimamisha kazi vigogo wake ili kupisha uchunguzi baada ya kubaini upungufu na ubadhirifu mkubwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Utalii (TDL) wa Sh.Bilioni nne.

Sambamba na hilo, imemuomba Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(Takukuru), kumchunguza aliyekuwa Mhasibu wa mfuko huo Eliud Kijalo na maofisa wote waliohusika na ubadhirifu huo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Msemaji wa Wizara hiyo, Dorina Makaya, Wizara hiyo kwa kushirikiana na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ilifanya ukaguzi maalum wa mfuko huo.

Makaya alisema katika ukaguzi huo Wizara imebaini upungufu na ubadhirifu huo na hivyo Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof.Adof Mkenda amechukua uamuzi mbalimbali ikiwemo kutengua uteuzi wa Mkurugenzi wa Utalii Deogratias Mdamu na kumsimamisha kazi ili kupisha uchunguzi.

"Pia Katibu Mkuu amemsimamisha kazi Flora Masami, Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Wizara ili kupisha uchunguzi," alisema.

Aidha, alisema Katibu huyo amemuagiza Kamishna wa Uhifadhi, Shirika la Hifadhi za Taifa(Tanapa) kumsimamisha kazi Moses Msemo aliyekuwa Mhasibu Mkuu wa Wizara hiyo ili kupisha uchunguzi.

"Pia Mkurugenzi wa Takukuru ameombwa kumchunguza Kijalo na wahusika wote, ambapo Kijalo tayari amekamatwa ili kusaidia upelelezi,"alisema.

Alisema Wizara hiyo itashirikiana na Takukuru ili wahusika wote wachukuliwe hatua stahiki na kwa haraka.

Katika taarifa ya Takukuru iliyotolewa na Ofisa Uhusiano wa taasisi hiyo Makao Mkuu, Doreen Kapwani, alithibitisha kumshikilia Mhasibu Mkuu wa mfuko huo, Eliud Kijalo kwa makosa ya ubadhirifu wa zaidi ya Sh. bilioni nne.

## HABARI KITAIFA

# Ushirika kusaidia jamii kwa mil. 36/-

**Na Happy Severine,** SIMIYU

CHAMA Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Simiyu (SIMCU) kimetenga Sh. mil 36.7 katika msimu wa pamba 2019/2020 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kijamii na kurudisha shukrani kwa wananchi .

Kati ya kiasi hicho, Sh 700,000 zimetumika kumsaidia mtoto Ritha Elias, mlemavu wa miguu kutatua changamoto ya usafiri na mahitaji yake ya msingi ya shule.

Akitoa taarifa fupi ya utekelezaji wa chama hicho jana, wakati wa kumkabidhi mtoto huyo baiskeli ya wenye ulemavu kwa ajili ya kutembelea, Kaimu Mwenyekiti wa SIMCU, Emmanuel Elias, alisema wameguswa kusaidia jamii katika kutatua changamoto zinazowazunguka.

Aidha, alisema Sh. milioni 24 zimetengwa kwa ajili ya kusaidia elimu na Sh. milioni 12 kwa ajili ya ununuzi wa mashuka katika hospitali zote za Mkoa wa Simiyu.

Awali akikabidhi baiskeli hiyo yenye thamani ya Sh. 400,000 kwa mtoto huyo pamoja na fedha taslim Sh. 300,000, Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alisema chama hicho kimefanya jambo kubwa na kutambua umuhimu wa kusaidia wenye ulemavu.

Nae bibi wa mtoto huyo, Ritha Elias, Perpetual Mtaima, alikishukuru chama hicho na uongozi wa Mkoa kwa ushirikiano waliouonesha kwa mjukuu wake.

# TFS yataka mapambano utunzaji mazingira

**Na Elizabeth Zaya**

> **Dunia inaadhimisha Siku ya Mazingira Duniani, hii ni kutukumbusha kwamba mazingira tuliyonayo ili yastawi lazima tuyatunze, na sisi kama taifa tuna wajibu wa kuhakikisha mazingira yetu tunayatunza na mwisho wa siku yanatoa huduma ambayo imekusudiwa,**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), imewaomba Watanzania na wadau mbalimbali kuongeza nguvu ya mapambano dhidi ya uharibifu wa misitu hiyo kwa ajili ya ustawi wa uchumi wa nchi.

Kamishna Mhifadhi wa Misitu Tanzania, Profesa Dos Santos Silayo, alisema uhifadhi na utunzaji bora wa misitu ni matokeo chanya ya kiuchumi kwa sekta nyingine ikiwamo ya mifugo, kilimo, maji na nishati.

"Dunia inaadhimisha Siku ya Mazingira Duniani, hii ni kutukumbusha kwamba mazingira tuliyonayo ili yastawi lazima tuyatunze, na sisi kama taifa tuna wajibu wa kuhakikisha mazingira yetu tunayatunza na mwisho wa siku yanatoa huduma ambayo imekusudiwa," alisema Profesa Silayo.

Alisema katika kipindi hiki cha kuadhimisha siku hiyo ni vyema kila mmoja akajijengea utaratibu wa kutunza mazingira hayo na kupambana kwa hali na mali dhidi ya vitendo vya uharibifu.

"Sisi kama TFS tunao wajibu wa kuhifadhi rasilimali za misitu, tunaamini ni muhimu kwa sababu inategemewa kwa uchumi wa nchi na pia kwa binadamu," alisema Profesa Silayo.

Aliwaomba wadau wote ambao wanahusisha na sekta hiyo ya misitu kuitumia Siku ya Mazingira Duniani kwa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na umuhimu wake na namna ya kuendelea kupambana na vitendo vya uharibifu.

# Sao Hill ilivyookoa mazingira kwa kugawa miche bure

**Na Francis Godwin, IRINGA**

MPANGO wa shamba la miti Sao Hill, wilayani Mufindi, mkoani Iringa kusaidia miche bure milioni moja kila mwaka wananchi wanazunguka msitu huo, umesaidia uboreshaji wa mazingira na ukuaji wa pato lao kiuchumi.

Mhifadhi Mkuu wa shamba hilo, Juma Mseti, akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu mkakati wa shamba hilo lililo chini ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), katika kuendelea kutunza mazingira, alisema pamoja na mkakati endelevu wa utunzaji wa mazingira ya asili, wanamkakati wa ukuzaji kipato cha wananchi kupitia misitu.

Alisema kila mwaka wanagawa miti milioni moja kwa wananchi wanaozunguka msitu huo kupanda kwenye maeneo yao na wengi wameitikia na kutekeleza.

Mseti alisema miti wanayoigawa ni aina mbalimbali ikiwamo ya nguzo za umeme, ya asili na mbao.

Alisema, upandaji miti umeendelea kuongezeka na kuwa Sao Hill wakiwa wadau wa mazingira, wanashiriki kuongeza kasi ya upandaji miti hekta 2,000 kila mwaka na jamii inayozunguka ikipewa miche ya bure.

Alisema kutokana na upandaji miti na utunzaji wa mazingira, wamechangia kupunguza kasi ya joto, pia kusaidia upatikanaji wa mvua ya uhakika.

Vile vile, shamba hilo limeendelea kuwa karibu na wananchi kwa kuangalia miradi yao na kuungwa mkono na walinzi wakubwa wa misitu hiyo isichomwe moto.

Mseti alisema, wakati huu wa janga la corona, wananchi Mufindi wametumia misitu hiyo kupata dawa ya kujifukiza.


AGRIBUSINESS INNOVATION CENTER AIC TANZANIA

PASS PRIVATE AGRICULTURAL SECTOR SUPPORT

**VITUO ATAMIZI VYA KILIMOBIASHARA VYA AIC TANGAZO KWA VIJANA**

**FURSA YA KUJIUNGA 2020/21**

Kituo cha Ubunifu wa Kilimobiashara (AIC), ambacho ni idara ya Taasisi ya PASS inapenda kuwatangazia vijana wenye nia ya kufanya kilimobiashara kwamba kinapokea maombi ya kujiunga na Vituo Atamizi vya Kilimobiashara vilivyopo SUA Morogoro na TALIRI Farm, Mbande, Kongwa mkoani Dodoma.

Katika vituo hivi, AIC inawapa fursa vijana ya kuanzisha, kumiliki na kuendesha kilimobiashara kwenye sekta ndogo ya mboga na matunda na mifugo na nyama.

Kijana atakayeomba nafasi hii anatakiwa awe na tabia njema, mtiifu, mwenye nidhamu, mchapakazi, fikra chanya, mwaminifu na anayependa kuona matokeo chanya. Vijana wa Kike watapewa Kipaumbele.

Vijana washiriki kwenye Vituo Atamizi watapewa vifaa, miundo mbinu, na mtaji wa kufanya kilimobiashara ambapo watausimamia kwa kipindi cha miezi 12.

Katika kipindi chote, waatainiwa watapewa usimamizi wa karibu ikiwemo ushauri wa kibiashara na upelembaji, ili kuhakikisha wanafanikiwa katika shughuli zao za kilimobiashara.

Baada ya kukamilika kwa muda huo, vijana watakaofanikiwa kwenye kilimobiashara, AIC itawawezesha kufanikisha kuanzisha biashara kama hiyo kwenye maeneo yao.

Vijana wenye nia wanashauriwa kutuma maombi yao ya kujiunga na kituo Atamizi kimojawapo kati ya SUA-AIC Morogoro kinachojihusisha na kilimobiashara cha mboga na matunda au AIC Kongwa kilichopo Taliri Farm (PRC), Mbande, Kongwa kinachojihusisha na biashara ya unenepeshaji/ufugaji mbuzi na usindikaji wa nyama ya mbuzi. Vijana 280 watachaguliwa kwenye awamu ya kwanza ya mchujo (200 kwa kituo cha Morogoro na 80 kwa Kituo cha Kongwa) na kati ya hawa, vijana 140 (100 Morogoro and 40 Kongwa) watachaguliwa kwenye awamu ya pili ya mchujo kujiunga na Vituo Atamizi kuanzia Oktoba 2020.

Kwa maelezo zaidi na jinsi ya kupata, kujaza na kurudisha fomu ya maombi yanapatikana kwenye tovuti ya www.aic.co.tz na www.pass.or.tz, SUA-SAEBS, ofisi za AIC (SUA, Morogoro na Mbande, Kongwa) na ofisi zote za PASS nchini.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 19/06/2020 saa 11.00 jioni.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wasiowalipa wanafunzi elimu ya juu wawajibike

**JUZI** Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alitoa saa 48 kwa vyuo vyote nchini ambavyo havijalipa wanafunzi fedha zao za kujikimu kufanya hivyo vinginevyo hatua zitachukuliwa dhidi yao.

Aidha, alieleza kuwa serikali imeshatoa Sh. bilioni 122 kwa ajili ya wanafunzi hao na zimeshapelekwa vyuoni, na kwamba wanaochelewesha ni vyuo vyenyewe.

Waziri huyo alieleza kuwa sababu inayotolewa na vyuo ambavyo bado havijawalipa wanafunzi, ni kwamba wengi bado hawajaripoti na kusaini nyaraka muhimu kwa ajili ya kupatiwa fedha hizo.

Alitaka waliosaini wapewe fedha wakati wengine wanaendela kuwaripoti, kuliko kuwachelewesha waliowahi kupata fedha hizo na kusoma kwa utulivu, huku wakihakikisha wanatumia vyema muda uliopo kwa kuwa ni mdogo kutokana na muda wa masomo kumezwa na muda waliokaa nyumbani kutokana na janga la corona.

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), ilishasema imeweka mipango ya utoaji wa fedha hizo na kilichokuwa kinasubiriwana mchakato wa vyuo na wanafunzi kurejea vyuoni.

Tunachokiona ni uzembe kwa baadhi ya vyuo ambavyo bado havijakamilisha suala la kuwapa wanafunzi fedha zao,na kuwafanya waishi maisha magumu kwa kuwa wanategemea fedha hizo kulipa kodi ya nyumba, nauli na chakula.

Kama hadi sasa hawajapewa fedha hizo wanaishije? maana yake kuna walioshindwa kuhudhuria masomo kutokana na kukosa mahitaji muhimu, ikiwamo chakula na hakuna ubishi mwenye njaa hawezi kusoma.

Kwa mazingira haya, ni rahisi wanafunzi hao kujiingiza kwenye mambo mengine yasiyofaa ambayo hayana afya kwa maisha yao ya sasa na baadaye, hivyo ni lazima vyuo vihakikishe fedha hizo zinawafikia wanafunzi kwa wakati.

Uwezo wa mwanafunzi kuelewa masomo na kufanya vizuri darasani kunaendana na kupata mahitaji ya msingi kama yalivyotajwa hapo juu, inapokuwa tofauti ni kutengeneza watalaamu legelege.

Kuchelewesha ni kurudi miaka ya nyumba, ambayo malalamiko na maandamano ya wanafunzi wa vyuo hayakukauka sababu kubwa ikiwa ni kucheleweshewa fedha za kujikimu.

Hakuna ubishi kuwa maandalizi ya wanafunzi kufungua vyuo yalishirikisha vyuo husika na ndiyo maana fedha zilipelekwa kufikia Mei 28, ambao ulikuwa muda mwafaka ili kuhakikisha wanazipata mapema na kutumia muda wao kwenye kusoma.

Kutokana na muda uliopotea kwa kukaa nyumbani, na masomo yaliyokuwa yafundishwe kwa wiki 17, sasa yatafundishwa kwa wiki 12 na wiki mbili za mitihani.

Maana yake muda uliopota ni wiki tatu ambazo zimesababisha mabadiliko makubwa kwenye kalenda za masomo, na sasa muda wa kusoma na kufundisha ukiongezeka.

Kupotea kwa wiki moja ni kwa sababu ya vyuo husika kushindwa kuwapa fedha wanafunzi, ni kuwanyima haki ya msingi ya kufundishwa na kujisomea kwa kuwa muda mwingi umetumika kufuatilia malipo, jambo ambalo lingetatuliwa na chuo husika kwa muda muafaka.


Vyuo vichukulie jambo hili kama wajibu wao na si hadi walazimishwe na Waziri, kwa kuwa fedha za wanafunzi zinapoingia moja kwa moja ni kusambaza kwenye akaunti za wanafunzi, kufanya hivyo kutaondoa usumbufu na kuwakwamisha kitaaluma.

Tunapenda kusisitiza vyuo hivyo visisubiri hatua kali za kisheria na kinidhamu dhidi yao, bali kuwajibika haraka na leo tusikie kila mwanafunzi wa kila chuo ampata fedha zake.

Tunaamini kuwa wakuu wa vyuo na watendaji wanahakikisha kuwa wanafunzi wanazipata fedha zao ifikapo leo kama serikali ilivyoelekeza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Maadhimisho haya ya mazingira yasaidie kumaliza biashara mkaa



Na Sabato Kasika

**NASEMA** haya nikisimama juu ya jukwaa la kilele maadhimisho ya leo, Siku ya Taifa ya Mazingira.

Hapo tunajua chanzo rahisi cha nishati ya kupikia, pia biashara kwa umma mijini na vijijini, kuna nishati mkaa.

Hiyo inahusisha wasambazaji wake wakubwa, rejareja na jumla. Kuna wanaopika majumbani, pia biashara; mamalishe na hotelini.

Kimsingi, mkaa ni chanzo kikuu cha nishati ya kupikia nchini. Pamoja na umuhimu wake huo, sasa kuna haja ya kuangalia matokeo ya ukataji miti kwa ajili ya kuchoma mkaa wa biashara.

Siyo siri kwamba ukataji miti kwa ajili ya kuchoma mkaa ambao unauzwa kwa ajili ya kupikia, unasababisha uharibifu wa mazingira, ikiwamo uwezekano wa maeneo yanayokatwa miti kubaki jangwa.

Biashara ya mkaa inashamiri kutokana na ukweli kwamba, gharama yake inaweza kuwa nafuu kuliko nishati nyingine, lakini ikumbukwe kuwa ukataji miti usiozingatia utaratibu, ni hatari kwa misitu na mazingira kwa jumla ambayo siku yake inaadhimishwa leo.

Mkaa umekuwa ukisafirishwa kwa baiskeli, pikipiki na magari, hivyo kila msafirishaji ana bei yake kulingana na gharama anayoitumia, usambazaji huo unaweza kuufanya mkaa kuuzwa kwa bei nafuu kuliko nishati nyinginezo.

Kwa hali hiyo, matumizi ya mkaa yatakuwa ni makubwa na kuna uwezekano wa kusababisha uharibifu mkubwa wa misitu, hivyo kuwapo changamoto nyingine za mazingira.

Uharibifu wa mazingira unaanza kule inakokatwa, inachomwa na mkaa unauzwa, hivyo ni muhimu wahusika wa biashara hiyo kuwa makini.

Biashara ya mkaa ni matokeo ya ukataji miti, pia unaweza kusababisha upotevu wa rutuba, upotevu wa mimea asilia, upotevu wa viumbe asilia, upungufu wa majisafi na salama.

Wakati huu wa maadhimisho ya Wiki ya Mazingira Duniani, ni muhimu wakataji miti kwa ajili ya kuchoma mkaa, watambue kwamba wanachangia uharibifu wa mazingira.

Mikoa kama vile Singida, Dodoma, Shinyanga, Manyara, Simiyu na Geita, imekuwa ikitajwa kuathiriwa na biashara ya mkaa, kwa vile inakumbwa na ukame na jangwa la ukataji miti ya mkaa.

Wakati umetimu sasa, nishati mbadala ufikiriwe namna ya kushusha bei Watanzania waweze kuipata kwa gharama nafuu.

Watu wanakimbilia kwenye mkaa, kwa sababu bado bei yake wanaweza kuimudu na umekuwa ukiuzwa kuanzia shilingi 1,000 kwa kipimo kuliko mafuta ya taa ambayo bei yake ni zaidi ya Sh. 1,000.

Hiyo ni bei kwa jiji kama Da es Salaam, ambako jamii imetakiwa ihamasishwe kupanda miti kwa wingi kwa kutumia kaulimbiu ya 'panda miti kata mti.' Utaratibu huo unaweza, walau ukasaidia kulinda mazingira ya nchi.

Vilevile wanaofanya biashara ya mkaa nchini wanapaswa kuzingatia matumizi bora ya mkaa katika misingi bora na endelevu, ili misitu iendelee kuwapo, ingawa inawezekana siyo suluhisho kamili la kumaliza jangwa.

Kiuhalisia, nishati mbadala ni suluhisho la yote. Kuna haja ya kujali na kuthamini umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa mazingira, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kulinda uoto wa asili.

Ipo kaulimbiu moja ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani iliyowahi kunadiwa 'Ardhi ni Makazi yetu Tuitunze kwa Manufaa ya Baadaye.' Hii ina maana muhimu sana, ikipingana na ukataji miti usiolingana na kiasi kinachopandwa.

Moja ya mambo ambayo Wizara ya Nishati, inahimiza, ni kuendeleza vyanzo vingine vya nishati ikiwamo umeme, gesi na mafuta, lakini bado matumizi yake hayajaenea kwa Watanzania wengi.

Ingawa marufuku biashara ya mkaa bado haijafikiwa, lakini uvunaji holela wa miti kwa ajili ya mkaa unaweza kuzuiwa, huku juhudi kuwapo kwa nishati mbadala zikiendelea kuchukuliwa.

# Matangi 100 kwa wanafunzi, wanavyuo Dar kinga corona

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imepokea msaada wa matangi 100 kutoka kampuni ya utengenezaji wa vifaa vya umeme ya Africab, kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi na wanavyuo jijini Dar es Salaam kunawa mikono ili kujikinga na ugonjwa wa virusi vya corona.

Akipokea msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 50, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema msaada huo umekuja wakati mwafaka wakati vyuo na baadhi ya shule nchini zimefunguliwa na kwamba itawawezesha wanafunzi kujikinga dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema msaada wa matangi hayo yenye ujao wa lita 1,000 kila moja yametolewa kwa shule 10 za sekondari za serikali na 57 kwa shule za sekondari binafsi na vyuo 13.

"Niwapongeze Africab kwa msaada huu muhimu kwa ajili ya kinga afya za wanafunzi wetu, niwaombe wadau wengine muige mfano huu kwa ajili ya manufaa ya watu wote wa taifa hili," alisema Prof. Ndalichako.

Alisema licha ya hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na serikali katika kupambana dhidi ya ugonjwa wa corona, wananchi nao wanapaswa kuchukua tahadhari hizo, huku wakiendelea kuchapa kazi.

Meneja Masoko wa Africab, David Tarimo, alisema msaada lengo la msaada huo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kukabiliana na ugonjwa wa corona na kusisitiza kuwa wao kama wadau wa maendeleo na wawekezaji wazalendo huo ni wajibu wao wa kimsingi.

Alisema mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona ni wajibu wa kila mmoja, na kwamba wao wanatambua nini kinafanywa na serikali katika kukabiliana na ugonjwa huo unaoisumbua dunia kwa sasa.

Alisema mbali na msaada huo, wataendelea kushirikiana na serikali katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo, huku ikitarajia kujenga kiwanda cha uzalishaji wa dawa za binadamu hivi karibuni.

Mkurugenzi Mwenza wa kiwanda hicho, Mohammed Ezz, alimshukuru Rais John Magufuli kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji yanayokiwezesha kiwanda hicho kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

# THRDC, LHRC wapinga kinga kwa Spika, makarani

**Na Enock Charles**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), umekosoa mapendekezo ya mabadiliko ya sheria ya bradea ambayo inasimamia haki za binadamu inayotoa kinga katika kushtaki baadhi ya viongozi.

Mabadiliko ya sasa yamtambua Spika wa bunge kuwa hawezi kushtakiwa moja kwa moja hadi kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, jambo ambalo wamedai linalenga kumlinda.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu, Onesmo Ole Ngurumwa alidai jana kuwa mabadiliko mengi ya sheria katika muswada namba tatu uliopelekwa bungeni hivi karibuni utapunguza haki za wananchi kujitetea mahakamani kuhusu haki mbalimbali na pia kuwapa kinga baadhi ya viongozi.

"Kwa mujibu wa mabadiliko haya ikiwa una malalamiko kuhusu Rais, Jaji Mkuu au Spika wa bunge malalamiko haya yatafunguliwa kupitia kwa Mwanasheria Mkuu, kwa mfano kama sasa hivi kuna kesi tumefungua dhidi ya Spika zote zinakwenda kuzuiwa," alisema Ole Ngurumwa.

Alisema kwa mujibu wa mabadiliko hayo, sasa itakuwa ni lazima kwa mtu kuwa na cheti cha kuonyesha namna alivyoathirika na ukiukwaji wa haki za binadamu, ili kuthibitisha madai yake mahakamani na pia kama mtu atakuwa na malalamiko dhidi ya viongozi wakuu wa serikali hataweza kufungua kesi ya moja kwa moja dhidi ya viongozi hao isipokuwa kwa kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Amelalamikia pia kitendo cha watumishi wa Mahakama wote ikiwamo makarani na wahasibu kupewa kinga ya kutoshitakiwa kwa jambo lolote jambo ambalo atalifanya akiwa anatekeleza majukumu yake mahakamani .

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alidai kuwa ni jambo la kushangaza kwa makarani na wahasibu wa mahakama kupewa kinga ya kutoshitakiwa mahakamani kwa kuwa watendaji hao hawana nguvu ya kimaamuzi na hivyo hakuna sababu yoyote ya kupewa kinga kama ilivyo kwa majaji wa mahakimu.

"Sisi tunaohudumia watu tunajua karani anaweza akapoteza faili lako kabisa na imetokea mara nyingi na wakipoteza tumekuwa tunawashitaki ,lakini sasa hivi maana yake ni kwamba hata akipoteza hawezi kushitakiwa," alisema Henga.

Alisema karani ambaye ndiye mtunzaji wa faili za kesi mbalimbali anaweza kukwamisha mtu kupata haki yake mahakamani kwa hiyo kwa kupewa kinga hiyo itapelekea haki za baadhi ya wananchi kupotea.



Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, Rodrick Mpogolo (kushoto), akimpokea Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha), mkoani Manyara, Elimiana Shishi (katikati) ambaye ni Diwani wa Viti Maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, aliyejiunga na CCM mjini Babati juzi. **PICHA GIFT THADEY**.

# Waliojenga msitu wa Selander kikaangoni

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, amekasirishwa na ujenzi wa nyumba katika eneo la msitu wa asili wa Selander jijini Dar es Salaam, na kutaka wachukuliwe hatua mara moja.

Alitoa agizo hilo jana kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini (NEMC) liwachukulie hatua watu ambao wamejenga na kufanya shughuli nyingine za kibinadamu katika eneo hilo.

Waziri alitembelea eneo la mikoko kando ya daraja la Selander baada ya kuwapo taarifa za kuendelea kwa shughuli za kibinadamu katika msitu huo wa asili ikiwamo ujenzi wa nyumba na utiririshaji wa majitaka baharini, wakati serikali inajenga daraja refu la kisasa ili kulifanya Jiji la Dar es Salaam liwe na mvuto wa kimataifa.

"Eneo la Selander ni miongoni mwa maeneo ya kimkakati katika utunzaji wa mazingira kama yalivyo maeneo mengine kote nchini yenye uoto wa asili. Eneo hili lipo ndani ya hifadhi ya mazingira na serikali haitakubali kuona shughuli zozote za kibinadamu zikiendelea katika eneo hili pamoja na maeneo mengine muhimu kote nchini," alisisitiza Waziri Sima.

Sima aliitaka NEMC kufuatilia kwa karibu watu wote ambao wamefanya shughuli za kibinadamu katika eneo hilo na kuwachukulia hatua za kisheria.

"Kumekuwapo na shughuli za kibinadamu katika eneo hili ikiwamo ujenzi na utiririshaji wa majitaka ambayo yanaingia baharini na kuleta madhara kwa viumbe wanaoishi majini. Naliagiza Baraza kuwatafuta watu wote ambao wamekuwa wakifanya shughuli hizo na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania kutunza mazingira ikiwamo maeneo maalum ambayo yametengwa na serikali kama sehemu ya maeneo ya uoto wa asili.

"Yanayofanyika hapa ndiyo yanayofanyika katika maeneo mengi yaliyotengwa na serikali nchini. Tumejipanga kuyalinda mazingira na yeyote atakayebainika kuyaharibu sheria itachukua mkondo wake," alisema.

Mkurugenzi wa Sheria wa NEMC, Benard Kongola, alieleza kuwa eneo hilo limekuwa na mgogoro kwa muda mrefu kidogo, na kwamba baraza limekuwa likichukua hatua kuhakikisha hakuna shughuli zozote zinafanyika katika eneo hilo.

"Pamoja na maagizo ya waziri ambayo tutayafanyia kazi mara moja, tunapendea ieleweke kwamba baraza limekwisha waripoti watumishi wa baraza ambao walishikiriana na wanufaika wa eneo hili kughushi nyaraka za kurasimisha eneo hilo kwa shughuli za kibinadamu," alieleza Kongola.

Amesema NEMC pia wamekuwa wakitembelea eneo hilo mara kwa mara kukagua mazingira ya eneo hilo na kuchukua hatua ikiwamo kuwapiga faini wanaotiririsha maji machafu baharini.




Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha NCCR – Mageuzi, James Mbatia, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu wa 2020, ikiwamo janga la ugonjwa wa corona na maandamano yanayoendelea nchini Marekani. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# NCCR-Mageuzi kutoa ratiba uteuzi wiki ijayo

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi, kimesema kitatoa ratiba ya uteuzi wa wagombea urais, wabunge, madiwani pamoja na wawakilishi, mwanzoni mwa wiki ijayo huku kikiitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kutenda haki katika uchaguzi mkuu 2020.

Pia, chama hicho kimefungua milango kwa chama chochote cha siasa nchini, ambacho kipo tayari kushirikiana ili kuiondoa Serikali ya Chama cha Mapinduzi madarakani.

Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia, alibainisha hayo jana wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma.

Mbatia alisema, tayari ameshamwagiza Katibu Mkuu wa chama hicho kutoa ratiba ya uteuzi wa wagombea ndani ya chama mapema wiki ijayo.

"Nitoe wito kwa vijana na wale wote wenye sifa, kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali, katika uchaguzi huu, nafasi za urais Tanzania bara na Zanzibar, ubunge, wawakilishi pamoja na zile za udiwani," alifafanua Mbatia. Alisema, katika uchaguzi mkuu mwaka huu, chama hicho kipo tayari kushirikiana na vyama vingine vya siasa kwa maslahi ya taifa.

"Sisi tupo tayari kushirikiana na chama chochote kile cha siasa kwa maslahi ya mama Tanzania, kwani hata salamu yetu inasema kwa pamoja tutashinda," alisema Mbatia. Alisema, katika uchaguzi mkuu 2020, ajenda yao ni Katiba mpya kwa kuwa ndiyo kauli ya umma wote.

"Ajenda yetu katika uchaguzi huu ni katiba mpya ni haki yetu kauli hii inatokana na umma wote lazima tutaendelea kuipigania kwa mslahi ya taifa letu," alisema.

AkizungumziaTume ya Taifa ya Uchaguzi nchini, alisema inatakiwa kuzingatia taratibu za kisheria na kikanuni na uamuzi yanatolewa kwa usawa na haki.

"Uchaguzi mkuu wa mwaka huu, mwezi Oktoba, tunataka kuliingiza taifa hili katika historia mpya kwa Tume ya Uchaguzi kutenda haki na usawa," alisema.

Aliwapongeza watu waliojiunga na chama hicho hivi karibuni, wakiwamo wabunge na viongozi wengine wakubwa.

Akizungumzia mlipuko wa virusi vya corona, Mbatia alisema wanaendelea kuwatahadharisha wananchi kuendelea kuchukua hatua ili kujikinga.

"Corona bado ipo, tuendele kuchukua tahadhari na kuondoa hofu mimi ni mtaalam wa majanga lazima tuhakikishe kuwa hofu yetu inaondoka kwa kuwa inachangia katika kushusha kinga ya mwili kwa kiwango kikubwa sana," alisema.

Alisema NCCR-Mageuzi, kinalaani vikali mauaji ya kikatili ya raia mweusi wa marekani George Floyd, akiwa mikononi mwa polisi hali iliyosababisha maandamo makubwa.

"Sisi kama taifa tuna kitu cha kujifunza, pia jeshi letu la polisi lina kitu cha kujifunza, maandamano haya yameathiri uchumi wa Marekani ambao unatugusa na sisi pia hapa," alisema.

# 193 washikiliwa kwa tuhuma uhalifu Pwani

**Na Julieth Mkireri, PWANI**

JESHI la Polisi Mkoa wa kipolisi Rufiji na Pwani linawashikilia watuhumiwa 193 kwa tuhuma za matukio tofauti ya uhalifu.

Akizingumza na wanahabari jana mjini Mkuranga Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Onesmo Lyanga, alisema watuhumiwa hao walikamatwa katika operesheni iliyofanywa na Jeshi hilo kuanzia Mei 29.

Lyanga alisema, 156 walikamatwa wakituhumiwa kuhusika na matukio mbalimbali yakiwamo ya uvunjaji, unyang'anyi kwa kutumia silaha na nguvu na wizi pamoja na utumiaji wa dawa za kulevya.

Alisema, katika oparesheni hiyo, vielelezo mbalimbali vimeanza kukamatwa ambavyo ni pikipiki sita, televisheni, deki, sabufa, kitanda cha mbao, vyoo vya kisasa viwili na simu za kiganjani mbili.

Alisema watuhumiwa wanane wameshafikishwa mahakamani na wengine watafikishwa uchunguzi ukikamilika.

Wakati huo huo, Kwa mujibu wa taarifa ya matukio kutoka kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, aliyoitoa jana mjini Kibaha, watuhumiwa 37 wametiwa mbaroni kwa tuhuma mbalimbali za uhalifu.

Wankyo alisema watuhumiwa 29 walikamatwa wakiwa na mbalimbali za wizi zikiwamo televisheni tatu, pikipiki 10 ambazo zinadaiwa zimebadilishwa chesis na injini namba.

Vitu vingine vilivyopatikana kwa madai ya kuibiwa na watuhumiwa hao ni rola ya waya mali ya Tanesco, magodoro, redio, mizani ya kupimia mizigo mizito, pombe, mihadarati na mitambo ya kutengeneza pombe ya moshi.

Alisema, watuhumiwa watafikishwa mahakamani baada ya uchunguzi kukamilika.

# Jafo ataka uwiano walimu mijini, vijijini

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

WIMBI la walimu wa shule za msingi na sekondari kurundikana katika shule zilizopo maeneo ya mijini limemshtua Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemeni Jafo na kuwaagiza wakuu wa mikoa kote nchini kuwapo uwiano mijini na vijijini.

Kauli hiyo aliitoa juzi wakati alipofanya ziara ya muda mfupi mkoani Mbeya ya kukagua ujenzi wa jengo jipya la Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, ukarabari wa shule ya kutwa ya Mbeya na kutembelea shule ya mchepuo wa Kiingereza ya Magufuli, jijini Mbeya.

Alisema pamoja na serikali kuajiri walimu 19,000, kuna changamoto ya walimu wengi kurundikana katika shule za msingi na sekondari maeneo ya mijini na hivyo kusababisha uhaba wa walimu usio na ulazima kwa baadhi ya shule zilizopo maeneo ya vijijini.

"Kuna walimu wengi wanaorundikana katika maeneo ya mijini na hii nawaagiza wakuu wa mikoa wote kuhakikisha mnatatua tatizo la walimu kujazana katika shule zilizopo maeneo ya mijini bila sababu yoyote na hivyo kuongeza ufanisi katika ufundishaji," alisema.

Waziri Jafo alitoa onyo kwa viongozi wa shule za serikali za mchepuo wa Kiingereza ikiwamo ya Shule ya Msingi Mkapa na Shule ya Msingi Magufuli jijini hapo ambazo zina mchepuo wa lugha ya Kiingereza kuwaandikisha watoto wenye sifa na kuacha kuendekeza rushwa kwenye uandikishaji.

Alisema kumekuwapo na vitendo vya ajabu kwa wasimamizi wa shule hizo na wazazi kujiingiza katika vitendo vya rushwa kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi hata wasiyo na sifa za kusoma katika shule hizo kuandikishwa na kuwa suala hilo halikubaliki na ni lazima viongozi waliopewa dhamana wakomeshe vitendo hivyo.

Alisema shule hizo zimekuwa na mchango mzuri kwa ajili ya maendeleo ya wanafunzi na nchi, wanafunzi wanaoandikishwa katika shule hizo ni lazima wawe na sifa zinazofanana na shule hizo.

Pia Waziri Jafo alitoa rai kwa wanafunzi wa kidato cha sita wanaotarajia kufanya mitihani yao mwishoni mwa mwezi Juni huu kuwa mitihani itakayokuja itajikita katika kupima ufahamu na uelewa wa mwanafunzi na kuwa wana wajibu wa kusoma na kuelewa maswali kipindi cha mitihani kitakapowazidia.

"Mitihani ya kidato cha sita kwa wanafunzi wanaotarajiwa kufanya itajihusisha kumpima mwanafunzi ufahamu na uelewa kwa kile alichosoma na itakuwa tofauti kidogo na miaka mingine," alisema Waziri Jafo.

# Wadaiwa masurufu kukatwa mishahara

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

UONGOZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, mkoani Tabora, umeagizwa kukata katika mishahara watumishi wanaodaiwa masurufi ya kiasi cha shilingi milioni 10.3 yaliyosababisha hoja ya kiukaguzi kutoka kwa Mdhibiti wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Agizo hilo limetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, wakati wa kikao maalumu cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo la kupitia hoja ya mbalimbali kutoka ripoti ya ukaguzi ya CAG kwa mwaka 2018/19.

Alisema ndani ya mwezi mmoja watumishi wote wanaodaiwa wahakikishe wamelipa fedha hizo au wakatwe kwenye mishahara yao.

Mwanri alisema wasipo katwa fedha hizo hoja hiyo itaendelea kujitokeza na kuchafua hesabu za Halmashauri hiyo wakati wa ukaguzi wa CAG.

Aliwataka wakuu wa idara kuhakikisha wamefanyia kazi hoja zote za CAG na kuwalisilisha vielelezo ili ziweze kufungwa.

Alisema watumishi ni vema wakajitahidi kutotoa maamuzi ambayo yanasababisha kuendelea kuzalisha hoja kila mwaka.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Mkoa amemwagiza Katibu Tawala Msaidizi (Serikali za Mitaa) kushirikiana na Mkurugenzi Mtendaji, Meneja wa RUWASA kuhakikisha wanaibana kampuni ya Drilling Ltd irejeshe shilingi milioni 23.5 baada ya kuchimba visima ambavyo havikuwahi kutoa maji.

Alisema fedha hizo zilipaswa kuwa zimerejeshwa tangu Septemba mwaka jana, lakini hadi sasa hakuna fedha zilizorejeshwa, na kuongeza kuwa ikiwa itashindwa kurejesha, waipeleke mahakamani.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga, Anamringi Macha (mwenye jaketi), akikagua namna ya mradi wa maji wa Mhungula Mlimani uliogharimu kiasi cha Sh. milioni 67, unavyofanya kazi, katika Kata ya Mhungula, wilayani humo jana. **PICHA: SHABAN NJIA.**

# Uboreshaji daftari Pemba wakamilika kwa changamoto

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

UBORESHAJI daftari la kudumu wapigakura awamu ya pili kisiwani Pemba imemalizika, huku ikikabiliwa na changamoto ya baadhi ya watu kukosa kitambulisho vya Mzanzibar kama sifa muhimu ya kuandikishwa kuwa mpigakura katika uchaguzi mkuu ujao kukosa kuandikishwa.

Baadhi ya mawakala kwenye vituo vya kura wamesifu kuwa zoezi limekwenda kwa utulivu mkubwa bila kuwapo misongomano, kutokana na baadhi yao kukosa sifa kwa kutokuwa na kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi, hivyo kushindwa kwenda kujiandikisha.

Acha Khamisi Hamad, wakala wa CCM, alisema zoezi lina utulivu mkubwa unaotoa nafasi kila anayepata kitambulisho kwenda na kujiandikisha mara moja, ila kunabadhi ya watu bado wapo lwenye afisi ya vitambulisho wakidai vitambulisho vyao.

Changamoto ya vitambulisho imekuwa na mitazamo tofauti kwa baadhi ya masheha na wananchi wa kawaida kutokana na upatikanaji wake.

Sheha wa Mtemani mjini Wete, Mrisho Haji mtwana (Magogo), alisema watu wengi hawafuatilii mapema vitambulisho vyao hadi wanaposikia uandikishaji na kujazana kwenye afisi za vituo, hivyo kuwapa wakati mgumu maofisa wa vitambulisho kutafuta kitambulisho cha mtu mmojammoja baada ya kuzongwa na kundi la watu.

Sheha wa Shengejuu, Faki Kombo, alisema baadhi wakishachukua vitambulisho huingia mitini kwa kusafiri na kuacha kujiandikisha kwenye daftari la kudumu, hivyo kufanya idadi ndogo ya wanaokwenda kujiandikisha mwaka huu.

Mkaazi wa Shengejuu ambaye Nipashe ilimkuta katika Kituo cha Shule ya Shengejuu, alisema watu wengi wanakata tamaa kufatilia wanapokwenda kituo mara moja au mbli na kukosa kitambulisho, hivyo kutokwenda tena na kukosa kujiandikisha.

"Mimi nilikwenda zaidi ya mara nne, na kila nikienda walikuwa wananiambia hakipo mara ya tano wakaniambia kipo, lakini hakisomi, nikaendelea kwenda hadi nilipofanikiwa kukipata na hatimaye kwenda kujiandikisha.

Aliwataka wananchi wasikate tamaa wanapokwenda kutafuta kitambulisho hadi kieleweke.

## Mil. 140/- kunufaisha vikundi h'shauri Nzega

**Na Tiganya Vincent,** NZEGA

HALMASHAURI ya Mji wa Nzega imetoa jumla ya shilingi milioni 140 kwa vikundi 40 ikiwa ni sehemu ya asilimia 10 ya mapato ya ndani.

Mikopo hiyo imekabidhiwa kwa vikundi hivyo jana mjini Nzega, ambapo Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Philemon Magesa, alisema vikundi 24 vya wanawake vimepatiwa mikopo ya shilingi milioni 74.5.

Aliongeza vikundi 11 vya vijana vimekopeshwa shilingi milioni 38 na vikundi 5 vya watu wenye ulemavu vimekopeshwa shilingi milioni 27.5.

Wakati huo huo Magesa alisema kuwa katika kipindi cha mwezi Januari mwaka huu walitoa mikopo ya shilingi milioni 70 kwa vikundi mbalimbali.

## Maabara magonjwa ya mifugo kujengwa

**Na Neema Emmanuel,** MEATU

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imepanga kujenga maabara 10 za kupima magonjwa ya mifugo kupitia bajeti ya 2020/2021.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wakati wa ziara yake ya kikazi Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu ya kukagua ukarabati na ujenzi wa josho la kuoshe mifugo la vijiji vya Mwakisandu na Isangijo, ujenzi wa maabara na kliniki ya mifugo ya Halmashauri ya Meatu pamoja na shughuli ya ukuzaji wa vifaranga vya kuku kijiji cha Mwandoya na jengo la wagonjwa wa nje OPD katika Kituo cha Afya Mwandoya.

Ulega alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inapunguza kwa kiasi kikubwa ueneaji wa magonjwa ya mifugo na kuyadhibiti, kwani wanataka kuhakikisha wafugaji wote nchini wanawahudumia kwa karibu.

"Kwa sasa tuna Kanda ya Mashariki, Kaskazini, Magharibi na Kanda ya Ziwa, lakini tunataka tuongeze ili huduma hiyo isogee karibu zaidi na kwa msingi huo, uzalishaji wa chanjo zile za kipaumbele mpaka sasa tumefanikiwa chanjo sita." alisema na kuongeza:

"Chanjo hizo ni za mdondo kwa kuku, kutupa mimba, chambavu. Vilevile tuna ya pamoja chambavu na ya kutupa mimba na chanjo ya homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP) hii ni chanjo ya karibuni ambayo inaendana na mazingira ya hapa kwetu tofauti na za nje ambazo zinahitaji majokofu kuzitunza."

# Kesi diwani wa CCM tuhuma za rushwa yapigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Temeke, imepiga kalenda kusikiliza maelezo ya awali katika kesi inayomkabili Diwani wa Kata ya Kijichi, Halmashauri ya Manispaa wa Temeke kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Elias Mtarawanje (29), mpaka Juni 15, mwaka huu.

Mtarawanje anakabiliwa na mashtaka mawili ikiwamo kushawishi na kupokea rushwa ya shilingi milioni moja kutoka kwa Yusuf Omary.

Mapema mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi, Catherine Madili, ilipanga kumsomea maelezo ya awali Juni 3, kigogo huyo wa chama tawala.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mwanakombo Rajabu, alidai Februari 6, mwaka huu, eneo la Mtoni Kijichi, Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa akiwa Diwani wa Kata ya Kijichi, aliomba rushwa ya shilingi milioni moja kutoka kwa Omary kama kishawishi ili asiweze kuzuia malipo ya fidia ya eneo jambo ambalo amelifanya tofauti na uhusiano wa shughuli za mwajiri wake.

Katika shtaka la pili, inadaiwa Februari 6, mwaka huu, eneo la tukio la Mtoni Kijichi, mshtakiwa huyo akiwa diwani kwa njia za rushwa alijipatia Sh. milioni moja kama kishawishi ili asiweze kuzuia malipo ya fidia ya eneo jambo ambalo amelifanya tofauti na uhusiano wa shughuli za mwajiri wake.

# Bil. 2/- kuwapelekea maji wakazi Musoma

**Na Sabato Kasika**

JUMLA ya Sh. bilioni 2.136 zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maji inayofanywa na Ruwasa katika Wilaya ya Musoma mkoani Mara, katika mwaka wa fedha wa 2020/2021.

Miongoni mwake ni upanuaji wa mradi wa maji ya Ziwa Victoria wa vijiji vya Suguti na Wanyere kwenda kijiji cha Saragana na kwamba hatua iliyofikia ni ununuzi wa vifaa.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Viencent Anney, alipokuwa akizungumza na gazeti hili na kuongeza: "Vilevile Ruwasa wanapanua mradi huo kuelekea katika vijiji vya Kata ya Nyambono, na pia kupeleka maji ya kisima katika vijiji vya Bugoji na Kaburabura."

Aliongeza kuwa Ruwasa watafanya usanifu wa mradi wa maji ya Ziwa Victoria kuanzia kijiji cha Chumwi kwenda vijiji vya Mabui Merafuru, Mikuyu na Seka.

"Miradi mingine kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 ni kuchimba visima na kufunga pampu za mkono katika vijiji vya Masinono, Muhoji na Kinyang'erere," alisema.




Kaimu Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Nyanda za Juu, Hamadan Silliah (kushoto), akikabidhi msaada wa mifuko 171 ya saruji kwa Mkuu wa Wilaya ya Momba, Juma Said Irando, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Makambini, mjini Tunduma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi Kahama wanufaika maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA) imetenga kiasi cha Sh. bilioni 1.2, kwa ajili ya kutekeleza miradi minne ya maji kwa wananchi wa vijiji na kata zilizopo pembezoni mwa mji, ambazo hazina huduma ya majisafi na salama.

Fedha hizo zinatokana na mapato ya ndani ya mamlaka hiyo na zilitengwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 kuanzia na miradi hiyo inatarajia kukamilika mwaka 2021 na kuhudumia zaidi ya kaya 15,080.

Akitoa ufafanuzi wa utekelezaji wa miradi hiyo kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, Meneja ufundi wa mamlaka hiyo, Mhandisi Luchanganya Paul, alisema lengo ni kuongeza mgandamizo wa maji na kusogeza huduma ya maji kwa wananchi.

Alitaja miradi hiyo na kiasi cha fedha kwa kila mradi kuwa ni Mwanva-Mbulu zaidi ya Sh. milioni 686, Mwendakulima Sh. milioni 47, Chapulwa Sh. milioni 445 na Mhungula Mlimani Sh. milioni 67.

Meneja wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Allen Mwara, alisema miradi hiyo inatekelezwa kwa fedha za mapato ya ndani.

"Mradi wa Mwanva-Mbulu mwanzo walitakiwa kutekeleza kwa kiasi cha Sh. milioni 915, lakini wanatekeleza kwa Sh. milioni 686 na kuokoa kiasi cha Sh. milioni 229," alifafanua.

Alisema kati ya kata 20 zilizopo Halmashauri ya Mji wa Kahama, kata 15 zimeshapata huduma ya majisafi na salama na kukamilika kwa mradi wa Ngogwa Kitwana ambao utahudumia zaidi ya kata tatu na itakuwa imefikia idadi ya kata 18 zenye huduma hiyo.

Kwa upande wake, DC Macha alipongeza mamlaka hiyo kwa kutekeleza miradi minne kwa wakati mmoja na kuwataka kuhakikisha ifikapo mwaka wa fedha 2020/21 kata mbili zinapata huduma ya maji kama ilivyo kwenye kata zenye maji.

Aidha, alilipongeza Gereza la Kahama kuchimba na kutandaza mabomba ya maji kama moja ya kuendelea kupunguza deni la maji wanalodai kwenye gereza hilo la zaidi ya Sh. milioni 140.

Mkazi wa Mbulu, Paulina Mabula, alipongeza mamlaka hiyo kwa kuwafikishia huduma ya maji kwenye makazi yao.

# NMB yasaidia ujenzi kituo afya cha corona

**Na Mwandishi Wetu,** TUNDUMA

BENKI ya NMB imekabidhi vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 5 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Makambini Halmashauri ya Mji wa Tunduma wilayani Momba mkoani Songwe kusaidia kukabiliana na janga la ugonjwa wa corona.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo kwa niaba ya Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu, Meneja wa NMB Tawi la Mbalizi Road, Hamadan Silliah, amesema msaada wa vifaa hivyo ni moja kati ya mpango wa NMB ya kutenga sehemu ya faida yake katika kusaidia huduma za kijamii.

Alisema walipokea maombi ya kusaidia ujenzi wa kituo hicho, na kwamba moja kati ya sera za benki ni kurejesha faida katika huduma za kijamii ni pamoja na kusaidia katika kukabiliana na majanga na huduma za afya.

Alisema kutanuka kwa huduma za benki hiyo kumeongeza pia uwapo wa huduma za NMB mkononi kupitia simu za kiganjani na hii imesaidia kufanya muamala kwa njia za kidijitali ikiwa ni moja ya sehemu ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Regina Bieda, alisema ujenzi wa kituo hicho kinachotarajiwa kuwa na wodi mbili za kinamama na wanaume kinatarajia kugharimu kiasi cha Sh. milioni 95.

Mkuu wa Wilaya ya Momba, Juma Said Irando, alisema kuwa benki hiyo imekuwa na mchango mkubwa katika huduma za kijamii na kuwa msaada katika kituo hicho cha afya ni mahsusi kwa magonjwa ya milipuko.

Alisema kituo hicho kipo mpakani ambayo ni njia kuu kuelekea nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Sadc), hivyo kumekuwa na mwingiliano wa wageni kutoka nchi zilizopo kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), na kuwa awali kituo hicho kilitengwa kwa ajili ya ebola na sasa kinaboreshwa kutokana na ugonjwa wa Covid-19.



Ukurasa 12

Wafanyabiashara, Mkurugenzi Jiji wanyoosheana kidole cha lawama




Ukurasa 13

Mbona bila vyama vya siasa inawezekana! -1

BUFE

IJUMAA JUNI 5, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

WAKATI SIKU YA MAZINGIRA...

# Msitu ulivyokamata uchumi taifa

## •Maelfu megawati umeme yaja

**Na Elizabeth Zaya**

***SEHEMU ya kwanza ya makala hii ilijadili nafasi ya misitu katika sura ya mazingira. Ufuatao ni mwendelezo wa sehemu ya tafsiri yake kiuchumi. Endelea:***

WAKATI leo ni maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, ni vigumu kutofautisha mazingira hayo na ustawi wa misitu.

Tanzania iko katika nchi zenye utajiri mkubwa kiuchumi wa milki ya misitu. Tathmini za mwaka 2009 na 2013 zinaonyesha upande wa bara, kuna takriban hekta milioni 48 za rasilimali hiyo.

Umuhimu wa misitu ni pamoja na vyanzo vya maji safi kwa matumizi ya nyumbani, viwandani, mifugo, kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji nishati umeme. Yote hiyo ni mitaji na malighafi ya kiuchumi.

Misitu pia inahifadhi viumbe vingi na aina mbalimbali; wanyamapori na uzalishaji mazao ya nyuki.

Iko bayana, wanyamapori wana mchango mkubwa katika utalii, wakati nyuki na viumbe wengine, hufanya kazi za kuchavusha maua na kusaidia uzalishaji matunda na mazao ya chakula.

Misitu, pia inasaidia kuzuia mmomonyoko wa ardhi, mafuriko na kwa kiwango kikubwa inadhibiti mabadiliko ya tabianchi inayoathiri sekta nyingi, hususani kilimo, mifugo na uzalishaji nishati umeme kwa kutumia maji asili.

**FAIDA KUU**

Takriban asilimia 34 ya misitu nchini, inasimamiwa na serikali, kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Eneo lingine la uchumi, misitu inasimamiwa na wadau kama mamlaka za wanyamapori (TAWA, TANAPA, NCAA), halmashauri za wilaya, vijiji, watu au kampuni binafsi na taasisi kama vyuo vya elimu, majeshi na taasisi za dini.

Wadau wanashauri kila mwananchi awajibike kuhakikisha anahifadhi na kulinda msitu, kutokana na faida zake kuu kiuchumi na kimazingira.



Mandhari ya panapojengwa mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere. **PICHA: MTANDAO.**

Hapo ndipo inazotajwa matokeo ya ujenzi wa Bwawa la Uzalishaji Umeme la Mwalimu Nyerere katika Mto Rufiji, ndani ya Pori la Akiba la Selous, ambalo sasa linajulikana Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

Ni tukio linaloingia katika orodha ya mafanikio ya mradi mkubwa kihistoria kiuchumi, inayotekelezwa na serikali iliyoko madarakani.

Inatarajiwa, bwawa hilo la kisasa lialoendana na uhalisia, litazalisha umeme zaidi ya megawati 2,115 inayoipa nchi faida kubwa ya umeme wa hakika na ziada, kwa gharama nafuu, mtaji wake ni ustawi wa misitu.

Faida nyingine, Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere, pia itaongeza matumizi ya umeme majumbani na hata kupunguza gharama ya uendeshaji viwandani.

Pia, kuna manufaa mengine yanayovutwa kutoka mlango wa pili kuhusu mazingira, kwamba itapunguza ukataji miti ya kutengeneza nishati mkaa, unaotumika zaidi kupikia.

Umeme wa uhakika na gharama nafuu, kiuchumi ina uwiano wa moja kwa moja na kuongezeka fursa za ajira, huku ikipunguza utegemezi wa mkaa na kuni.

Hapo maandiko ya mradi huo, yanabeba tafsiri kwamba, itaongeza kasi ya maendeleo kwa uanzishaji viwanda vingi vya kutengeneza vifaa mbadala vya ujenzi na kupunguza utegemezi wa mazao ya misitu, hususani mbao.

Mradi wa kitaifa wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), ulioko sasa awamu ya tatu, matarajio ni kuona ukombozi wa kupatikana umeme wa uhakika na gharama nafuu vijijini, dira kuu ni hakuna kijiji kinachopaswa kuachwa.

Kwa mujibu wa mtazamio hayo, kwamba umeme wa uhakika na gharama nafuu, unapunguza uharibifu na uharibifu misituni.

Kurejea Mradi wa Nishati wa Julius Nyerere, ni kwamba Watanzania wanatazamia neema ya kuongezeka kipato na maisha kupanda ngazi zaidi.

Ndani ya angalizo hilo kiuchumi kutoka matazamio ya mradi, Watanzania wanapopanda daraja kimaisha, ina maana maisha na uwezo wao wa kuchagua na kumudu nishati mbadala, itawasaidia kupunguza utegemezi wa mkaa.

Vivyo hivyo, itaendana na kuongeza matumizi ya pembejeo na kujiepusha na kilimo cha kuhamahama, hali inayookoa misitu ambayo inaathirika hadi sasa.

**WADAU MISITU**

Wadau misitu wana maoni, uwapo wa Mradi wa Julius Nyerere, utapunguza uharibifu, pia ni mchango mkubwa katika kutekeleza itifaki ya kimataifa ya mabadiliko ya tabianchi, inayozitaka nchi zichangie kupunguza mabadiliko ya tabianchi na uharibifu misitu.

Ni zao ambalo likifanikiwa, hapana shaka itasaidia kuboresha misitu kwa manufaa ya maendeleo ya sekta nyinginezo kama vile kilimo, maji, mifugo, uvuvi, viwanda na uzalishaji umeme.

Mradi wa Bwawa la Julius Nyerere, wadau wa misitu wanalieleza ikitunzwa chini ya pazia ya ulinzi wa misitu, una faida nyingi kuanzia kitaifa, hadi mwananchi mmoja mmoja.

**CHANGAMOTO JE?**

Juhudi za TFS zimekuwa zikikutana na changamoto katika usimamizi wake, kuu ni upotevu wa misitu.

Utafiti uliofanywa na wadau wa misitu, unaonyesha takribani hekta 450,000 hupotea kila mwaka, kutokana na kuftekwa kuzalisha mkaa.

Kwanini hivyo? Jibu ni kwamba kila sehemu inakimbilia nishati mkaa, sababu kuu ni gharama ya nishati mbadala kama majiko ya gesi na umeme, elimu duni ya mazingira na utamaduni wa kihistoria.

- ***Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa za kitafiti kuhusu misitu.***

Mwisho.

BIASHARA

KUDODA SOKO KUU MWANZA

# Wafanyabiashara, Mkurugenzi Jiji wanyoosheana kidole cha lawama

- Hakuna umeme, mifereji, wala geti
- Wengi wakimbia kuhamia 'machinga'

**Na Anthony Gervas, Mwanza**

KWA mkazi wa jiji la Mwanza au wageni wenye uenyeji nako, wanalifahamu vyema Soko Kuu la Muda Mbugani. Ni mradi mkubwa, uliokuwa na shauku lakini ulikoishia sasa kitendawili.

Iko wazi na wote wanakiri pana shida. Miundombinu haiendani na mahitaji kibiashara, malalamiko yametawala, baadhi ya wafanyabiashara wanakimbia, kibaya zaidi uchafu wa mazingira na mifereji, kukosekana umeme ni malalamiko yasiyo na kikomo yakidumu miezi tisa sasa.

Nini mzizi wa shida? Wakati wafanyabiashara wanajiona wapangaji waliokaribishwa baada ya kuhamishwa kutoka kwingine, hivyo hawawajibiki na gharama yoyote, mwenye mali Halmashauri ya Jiji Mwanza, inaliona kivingine.

Mtazamo wa Jiji umegawanya katika 'mikono' mikuu mitatu; inajipa hisa kidogo kugharamIa, sehemu zilizobaki, wafanyabiashara wawajibike na nyingine inakinga mkono wa msada kwa serikali kuu.

Ni hoja tata iliyoifanya Nipashe itumie kanuni ya kisheria maarufu 'Natural Justice' kwa maana ya kila upande kusikilizwa kujua nini hasa kilichojificha hata mradi huo ukadoda?

Safari ilianzia ushuhuda sokoni na kubaini biashara ngumu, kukatika mitaji, wafanyabiashara wanakimbia vyumba, pia meza za kuuza mboga na matunda wakirejea mitaani, bucha za nyama hazina umeme na bidhaa zake haziishi siku moja.



Katibu wa Soko la Migahawa na Mamalishe, Agnes Lawrance, akipika chakula cha wateja.



Katibu wa Soko Kuu Mbugani, jijini Mwanza, Kurwijira Makubi, akiwa ndani ya soko baada ya kumtembeza mwandishi.

**WAHUSIKA SOKONI**

Mwenyekiti wa Soko Kuu la Mbugani, Hamad Nchola anasema, soko hilo halina umeme tangu walivyohamishiwa hapo Septemba 28 mwaka jana, kutoka Soko Kuu la zamani kupisha mradi wa Halmashauri ya Jiji Mwanza, kujenga soko la kisasa.

"Tunaomba Serikali tukae chini ili kufikia mwafaka kupata huduma stahiki katika soko hili, umeme hakuna, mifereji ya kupitisha maji machafu hakuna, hali ni mbaya, hata walinzi wananawajibika gizani kwa kutumia tochi.

"Milango ya mageti kwa ajili ya kufunga soko haipo, jambo linalohatarisha usalama wa maisha ya wafanyabiashara na mali zao, ikiwamo kukatika mitaji yao," analalamika Mwenyekiti .

Nchola, huku akiomba mjadala wa meza moja na serikali kutafuta ufumbuzi, anadokeza athari zilizojitokeza, baadhi yao wameshakimbilia mitaani kila mmoja anakoweza, baadhi wamejiunga na u-machinga.

Anatoa takwimu, zaidi ya meza 20 za wauza mboga na matunda, vyumba vya maduka takribani 30, pia migahawa na mamalishe sokoni zimeachwa, kwa madai ya ugumu wa biashara, utokanao na uhalisia aliyoutaja.

> **"Wakati tunahamishiwa huku tangu mwaka jana, tuliambiwa huduma zote muhimu zitakuwapo, ikiwemo umeme, lakini tulipokuja tulikuta tofauti na makubaliano yetu. Umeme hakuna wakati soko la zamani waling'oa hata mita zetu za umeme na hadi sasa hatujui ziko wapi.**

Wambura Masiaga, mfanyabiashara maarufu wa nyama, anaeleza changamoto yao ni kukosekana umeme, mifereji ya kupitisha majitaka na soko kukosa mageti ya usalama wa mali zao.

"Wakati tunahamishiwa huku tangu mwaka jana, tuliambiwa huduma zote muhimu zitakuwapo, ikiwemo umeme, lakini tulipokuja tulikuta tofauti na makubaliano yetu. Umeme hakuna wakati soko la zamani waling'oa hata mita zetu za umeme na hadi sasa hatujui ziko wapi.

"Nyama zikibaki hatuna pa kuzitunzia zinaoza na biashara ni mbaya. Mwanzoni tulipokuwa soko kuu la zamani, tulikuwa kila mmoja akinunua ng'ombe mzima wa kuchinja, lakini hivi sasa tunanunua nyama machinjioni kilo 30 au 40 kulingana na hali ya biashara wateja hakuna," anasema Masiaga.

"Hali hiyo imesababisha maisha yetu kuwa magumu, mitaji kukatika na kama itaendelea hivi bila serikali kuchukua hatua ya kutusaidia, tutafunga biashara hizi na tukafanye zingine.

"Jiji walituingiza 'chaka' tukaingia mkataba wa kujenga vyumba vya kuuzia nyama kila mmoja. Mimi nimetumia zaidi ya Sh. milioni nne kujenga chumba hiki," analalamika.



Meza za wauza mboga na matunda sokoni zilizotelekezwa. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**

Kwa mujibu wa Masiaga, mkataba wa ujenzi wa vyumba hivyo ililenga kukatana na jiji kodi ya pango kila mwezi ingawa hawajaanza, wakisubiri kupewa utaratibu.

Anasema hivi sasa kuna mgawanyiko, baadhi yao wamehama kutoka ndani ya soko na wanauzia nje na hata uchochoroni.

Agnes Lawrence, ni Katibu wa Migahawa katika soko hilo, anayepaza sauti yake kuwa mazingira wanayofanyia biashara ni machafu na kukosekana mifereji ya kupitisha majitaka, inawapa wakati mgumu kupata wateja.

"Soko hili ni chafu halina hata mifereji ya kumwaga maji machafu, wateja wamekuwa wakiona kinyaa kuja kula humu biashara sasa ni ngumu na wengi kama unavyoshuhudia mwandishi wametelekeza vyumba vyao," anasema.

Agnes anataja athari kuu iliyopo sasa ni mitaji yao imetetereka, baadhi wakiwa kwenye mikopo na hata sasa wanaingia katika mitihani ya kuirejesha, pia ushuru na kodi serikalini.

Kwa mujibu wa Agnes, bei ya vyakula walivyouza kati ya Sh.1500 hadi Sh. 5,000, sasa bei imeangukia wastani kati ya Sh.1000 hadi Sh. 2000 huku mzigo wa chakula ukibaki kila siku na wanashindwa kuwalipa wasaidizi wao.

**KATIBU SOKO**

Katibu wa Soko, Kurwijira Makubi, anaiomba serikali kuwarejesha wafanyabiashara waliotelekeza sehemu zao na kukimbilia mtaani, ili waweze kukaa sehemu kupata wateja.

"Sisi hatupati wateja sababu wengi wanapata huduma huko huko mtaani na vichochoroni," analalamika kwamba ni kinyume na makubaliano kabla ya kuhamia hapo, wafanyabiashara walikusanyika hapo, sasa wamegawanyika wakitapatapa kusaka masoko

Katika kundi hilo, anasema kuna waliotelekeza vibanda vya biashara walivyovijenga sokoni na mardhiano yao ni kodi ambayo haijaanza kukusanywa ya Sh.10,000 kwa mwezi kwa kila mfanyabiashara

**MKURUGENZI JIJI**

Ni makusanyo ya hoja, ambayo Nipashe iliwasilisha mezani kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Kiomoni Kibamba, ili kupata ufafanuzi serikalini .

Anasema: "Soko kuu la muda tulilowahamishia wafanyabiashara hao, jukumu la kuweka umeme ni lao, kwa sababu biashara ni zao sio za serikali. Sisi kazi yetu ilikuwa kuwapelekea nguzo, ili wavute umeme wenyewe na nguzo zipo."

Katika dai la mazingira machafu sokoni na kukosekana mifereji, Mkurugenzi anasema aliwapelekea 'moramu' ya kufukia maeneo korofi, lakini wafanyabiashara akidai walitamka: "Kazi hiyo ifanywe na serikali yenyewe iliyotuhamishia eneo hilo."

Anaendelea kwa kuwahoji: "Sasa mimi nifanyeje, wanataka nipeleke 'moramu' na kazi niwafanyie?... lakini wakikubali, hata kesho tu nawapelekea! Hata wale waliotelekeza vyumba vyao sokoni tumejaribu kuwarudisha, wamegoma wakiwamo 'machinga,' sasa tufanyeje sisi (serikali)?

"Lakini, watu wanasifia kuwa soko limechangamka kweli kweli sasa hivi, biashara ni nzuri, waliotelekeza vyumba, meza na vibanda tutawapa watu wengine," anafafanua Kabimba.

Kuhusu uboreshaji miundombinu ya soko na ujenzi wa mifereji ya kupitisha maji machafu, umeme na milango ya mageti, anasema inahitaji kiasi cha Sh. milioni 315, fedha ambayo Halmashauri ya Jiji la Mwanza halina na limeelekeza ombi serikali kuu, ikisubiri bajeti ijayo.

**SOKO JIPYA?**

Mkurugenzi Kabimba anasema, ujenzi wa soko jipya uliofanya wafanyabiashara hao kuhamishiwa waliko sasa katika iliyokuwa Shule ya Msingi Mbugani, ulitarajiwa kuanza mwaka jana, lakini ukakwama.


"Hatujaanza ujenzi wa soko kuu ambalo litakuwa la kawaida sio la ghorofa kwa sababu hatuna fedha. Hivi sasa tunasubiri bajeti ya serikali ya mwezi Julai, itakapopitishwa ndipo tutaanza ujenzi wake. Kwa sasa hatuna fedha na ujenzi huo, unahitaji kiasi cha Sh.bilioni 15," anasema.

Anatoa wito wafanyabiashara hao kuwa wavumilivu katika biashara katika kipindi cha mpito cha ujenzi wa soko jipya.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Mbona bila vyama vya siasa inawezekana! -1






**NA JOSEPH KULANGWA**

HII nchi ilikotoka ni mbali mjue. Ilitawaliwa kichifu na kisha kikoloni na hatimaye ikajitawala. Enzi za uchifu, koo ziliachwa zijiongoze, zikichagua, kuteua au kurithisha uongozi.

Enzi hizo ukizaliwa kwenye ukoo wenye chifu au mtemi au mtwa, basi ujue nawe siku moja utaongoza ukoo au kabila.

Walipokuja Wazungu, kwa akili zao wakatuona sisi na uongozi wetu ni hatuna maana na hatujastaarabika, huku wakijua fika kwamba tulikuwa na taratibu zetu za kuabudu kiimani. Wakasema fikra duni zetu ndio zilitufanya kuabudu miti, miamba, mito, milima na wanyama.

Kwa mahubiri na mafunzo yao, Wazungu hao wakatupatia imani zao na kutuaminisha kwa njia ya dini, kwamba hicho tuaminicho ni uduni wa mawazo na si ustaarabu, wakatupiganisha, nasi tukaacha kuamini yetu, tukashika yao.Tukashika dini, tukaacha kutambikia tukakimbilia kwenye mapya.

Tukajengewa hofu kwamba tukikosa na kupigana, tutakuwa tunamkosea Muumba wetu ambaye ni mmoja. Tukaachana na tulikoamini.

Tukawaamini waliokuja kwa nyadhifa za majina maalum, wakatujengea na tukaabudu humo. Kweli tukamwogopa Muumba, tukiishi kwa kushirikiana na mgeni huyo.

Tukaishi hivyo, tukitumika kuwazalishia, hadi hapo tulipokuja kutanabahi kuwa tulikuwa tukitumikishwa kwa maslahi yao.

Tukajitambua kuwa kumbe sisi tulikuwa watumwa wa mabwana, tukishughulishwa na kuuzwa kama bidhaa kwa maslahi yao.

Tukaendelea kuzalisha na mazao yetu kuchukuliwa, yakipelekwa walikotoka, kwenda kutengenezea bidhaa ambazo hatimaye zilirudi kwetu na kutolewa zawadi kwa viongozi wetu, ili waendelee kutuuza na zingine tukiuziwa jasho letu.

Dunia ikaendelea kubadilika, hadi tulipotambua kuwa kumbe tunanyonywa na sasa tunaweza kujiongoza wenyewe. Hiyo ilitokana na elimu ya shuleni tuliyopewa na wageni hao ambao hata hivyo, ililenga kusomesha watoto wa viongozi.

Elimu hiyo ikatujuza kuwa hatukustahili kuwa watumwa wa kutumikia wageni wakati ardhi ni yetu na ni haki tuliyopewa na Mungu, ambaye ni wao walituaminisha kwake. Tukakataa, tukapambana na kuwaondoa wakarudi kwao na si tukashika hatamu.

Tuliwaondoa kwa kuanzisha vikundi vya pamoja, ambavyo baadaye vikaja kuitwa vyama, vikilenga maeneo ya makazini na mashambani na hatimaye vikawa vya kisiasa. Hawa wakawa na chama na wale wakawa na cha kwao.

Hiyo ilitokana na sisi wenyewe kutazamana vibaya, kwamba hawa wanajiona bora na wastahiki nafasi za wageni hao au Wakoloni.

Vyama vikawa vingi na hatimaye vikawa vinapamba na kupata kiongozi wa vingine. Ukafanyika uchaguzi. Historia ni ndefu, lakini hatimaye TANU ikashinda. TANU ni kifupi cha Tanganyika African National Union.

Kikaongozwa na Mwalimu Julius Nyerere na kuleta uhuru wa Tanganyika mwaka 1961.

Baadaye tukaona ni bora kuwa na chama kimoja tu, ili kudumisha umoja na mshikamano wa Watanganyika. Majirani zetu Zanzibar nao wakaona umuhimu huohuo, kukawa na chama kimoja cha ASP, yaani Afro Shirazi Party.

Nacho kikadumisha mshikamano wa Zanzibar baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 yaliyoondoa usultani.

Suala la umoja likahanikizana hivyo mwaka huo huo wa 1964, Jamhuri za Tanganyika na Zanzibar zikaungana na kuzaa Tanzania. Mwalimu Nyerere wa TANU akawa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, huku Shekhe Abeid Amaan Karume wa ASP, akiwa Makamu wa Rais.

Na kweli, Tanzania ikawa moja na yenye utulivu mkubwa, kuthibitisha kuwa kweli Watanganyika na Wazanzibari kihistoria ni ndugu na wamoja. Hali hiyo ikasababisha kuzaliwa wazo la kuunganisha vyama hivyo na kuzaliwa CCM, yaani Chama Cha Mapinduzi, mwaka 1977.

Hakuna lililoharibika, mambo yakaendelea kushamiri na kunyooka, ukienda Visiwani ni njano na kijani ukirudi Bara ni njano na kijani.

Nchi moja chama kimoja cha siasa, Bunge moja chama kimoja. Wabunge wakawa na kambi moja wakijadili maslahi ya nchi kwa umakini mkubwa.

Walikataa jambo kwa umoja wao na kulikubali kwa umoja wao.

Mambo hayakuwa rahisi rahisi katika kupitisha bajeti na miswada, eti kwa sababu wabunge wote walikuwa wa chama kimoja, la hasha, walikabana kweli kweli mpaka mwisho ili kulinda maslahi mapana ya nchi na watu wake.

Shilingi iliondolewa kwenye mshahara wa Waziri mpaka kieleweke.

Baada ya miaka takriban kumi na ushei hivi, vuguvugu na mabadiliko ya kisiasa likaibuka duniani, wimbi la kuwapo kwa mifumo wa vyama vingi duniani, likasambaa na kuikumba Afrika. Tanzania hatukuwa kisiwa. Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi akaona isiwe shida, akaunda Tume ya kutafuta maoni ya wananchi kuhusu mfumo wa vyama vingi.

**•Simu: (+255) 0713 410008 na baruapepe: jkulangwa@yahoo.com**

MAKALA MAALUM

# SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI NA VITA KUTOKOMEZA COVID-19



Askari wa vikosi vya ulinzi na usalama, wakishiriki kukabili athari za mazingira, iliyotokea katika ufukwe mkoani Mtwara.

**Na Mwandishi Wetu**

KILA tarehe 5 Juni, nchi yetu hungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Sikuya Mazingira Duniani. Maadhimisho ya Siku ya Mazingira duniani yaliamuliwa mwaka 1972 katika mkutano wa kwanza wa Umoja wa Mataifa uliohusu masuala ya Mazingira, uliofanyika katika Mji wa Stockholm nchini Sweden. Mkutano huo uliazimia kwamba tarehe 5 Juni, kila mwaka iwe ni siku ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yanatoa nafasi ya kutafakari kuhusu hali na umuhimu wa hifadhi ya mazingira katika nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa,

kuelimisha wananchi kushiriki katika shughuli za hifadhi ya mazingira na mbinu mbalimbali za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kuenea kwa hali ya jangwa na ukame, Upotevu wa bioanuai, uharibifu wa tabaka la ozone, na shughuli nyingine mbalimbali zinazochangia uharibifu wa mazingira

Akiongea katika taarifa yake aliyotoa kwa vyombo vya habari Waziri wa Nchi Ofisi ya

Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Zungu alisema kuwa Taifa linakabiliwa na changamoto kubwa ya uharibifu wa mazingira unaotokana na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za kimazingira.

Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na uharibifu wa ardhi, ufyekaji na uharibifu wa

misitu, uharibifu wa vyanzo vya maji, uharibifu wa makazi ya viumbe wa majini na upotevu wa bioanuai. Changamoto hizi kwa ujumla zinasababisha athari kubwa katika masuala ya kiuchumi na kijamii. Katika kukabiliana na changamoto hizi

> **“Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Zungu alisema kuwa Taifa linakabiliwa na changamoto kubwa ya uharibifu wa mazingira unaotokana na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za kimazingira.**



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, akizungumza ofisini kwake. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kupambana na hali hii. Mojawapo ya njia za kupambana na changamoto hii ni kutumia Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ili pamoja na mambo mengine kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa maendeleo endelevu.

Kaulimbiu ya maadhimisho haya kitaifa ni Tuhifadhi Mazingira: Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi. Kaulimbiu hii inaakisi hali halisi ya nchi yetu kuathirika na

mabadiliko ya tabianchi. Katika miaka ya hivi karibuni nchi imeshuhudia kuongezeka kwa matukio ya ukame mkali na wa mara kwa mara pamoja na mafuriko ambayo yamekuwa yakiikumba nchi yetu na kusababisha hasara kubwa ya miundombinu, makazi ya watu na hata vifo katika baadhi ya sehemu.

**ATHARI ZAKE**

Hivi karibuni mafuriko yaliyoukumba mkoa wa Lindi na kusababisha hasara kubwa, takriban vijiji 16 viliathiriwa na mafuriko hayo pamoja na watu 19 kupoteza maisha kutokana na mafuriko hayo.

Aidha, takriban watu 15,000 wamekosa makazi pamoja na uhaba wa chakula na kuathiriwa na magonjwa mbalimbali ya mlipuko.

Kaulimbiu hii inahimiza jamii kutumia mbinu mbalimbali za asili na za teknolojia rafiki za

kuhifadhi mazingira ikiwemo kilimo cha matone, nishati mbadala, ufugaji wa mifugo chotara na upandaji wa miti ya asili kwenye vyanzo vya maji ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi nchini.

Katika Taarifa hiyo Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Zungu, aliongeza kuwa Tanzania na dunia kwa ujumla, zinakabiliwa na janga la ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Ni ugonjwa unaoambukizwa kwa njia mbalimbali ikiwemo mikusanyiko ya watu. Uwepo wa janga hilo, umesababisha kusitishwa kwa shughuli zinazohusu mikusanyiko ya watu.

Aidha, kutokana na hali hiyo, serikali imeamua kwamba mwaka huu hapatakuwapo na

mikusanyiko kwa ajili ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Kitaifa, yaliyopangwa kufanyika mkoani Lindi.

Kwa muktadha huo, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo, wamekubaliana kuwa maadhimisho ya wiki ya Siku ya Mazingira Duniani yatafanyika kwa kutumia vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii kuelimisha na kuhamasisha jamii kutunza mazingira na kuzingatia njia mbalimbali za kujiepusha na maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Aidha, kila mkoa utafanya shughuli za maadhimisho hayo kwa kutumia vyombo vya habari vilivyopo kwenye maeneo yao pamoja na mitandao ya kijamii kwa kuzingatia kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ikiwa ni pamoja na:

mashindano ya kuandika insha zinazohusu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, hotuba za viongozi, ujumbe mbalimbali utakaotumwa kwenye mitandao ya simu pamoja na mikutano ya kitaalamu kuhusu mabadiliko ya tabianchi itakayofanywa kwa njia ya mitandao kwa kuzingatia njia mbalimbali za kujiepusha na maambukizo ya ugonjwa wa corona.

**MKUU WA NEMC**

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira

(NEMC) Dk. Samuel Mafwenga, katika kuadhimisha Siku ya Mazingira ya Duniani aliwasisitiza wananchi kuendelea kutunza mazingira kwa kupanda miti,kutunza

vyanzo vya maji na kuzingatia kwa umakini sheria na taratibu za kuhifadhi mazingira ili kuepuka athari ziletwazo na mabadiliko ya tabianchi.

“Tuendelee kuyatunza mazingira yetu kwa kutunza vyanzo vya maji maana vingi


vimeharibiwa, tuache kukata miti, ili kuepuka madhara ya mabadiliko ya tabianchi,”alisema Dk. Mafwenga.

Inafahamika, hifadhi ya mazingira si kazi ya serikali pekee yake bali ni jukumu la kila mmoja katika jamii. Kila mmoja katika kaya ana wajibu na fursa muhimu ya kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira kitaifa.

Kushirikiana , inahusu masuala kama kupambana na kukabilianadhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hivyo, kila mwananchi ana wajibu katika nafasi yake, kulinda mazingira kwa ujumla.

Mkuu wa NEMC anakumbusha shughuli za maadhimisho ya Siku ya Mazingira nchini mwaka huu, zitalenga kuhamasisha jamii kuhifadhi mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuelimishana jinsi ya kuepuka maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19.





# Soko la Ndugai, stendi mpya rasmi Jumatatu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameagiza kuanza kutumika kwa Soko Kuu la Ndugai, kituo cha mabasi na maegesho ya malori ifikapo Juni 8 mwaka huu (Jumatatu) kutokana na kukamilika kwa ujenzi wake.

Alitoa agizo hilo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo mikubwa.

Alisema ujenzi wa miradi hiyo umekamilika na kuagiza huduma za usafiri katika kituo cha mabasi yaendayo mikoani kilichoko Viwanja vya Nanenane kuhamishiwa kwenye kituo kipya.

"Terminals' zote zilizokuwa zinatumika, tunazipa muda wa siku 30 ili nao wahamie stendi mpya na 'terminals' zao zitabaki na kazi ya 'service' za magari yao tu," alisema.

Dk. Mahenge alisema viwanja wa Nanenane vitaendelea kuwa kituo cha daladala, lakini kutakuwa na kituo cha daladala kwenye soko na kituo kipya cha mabasi.

Alisema baada ya kujengwa kituo maalum cha daladala, shughuli za daladala zote zitahamia huko na viwanja vya Nanenane vitabaki kwa ajili ya shughuli za wakulima na wafugaji.

Alisema maegesho ya malori yako eneo la Nala na yana uwezo wa kuegesha malori 300 yenye zaidi ya tani tatu, hivyo ifikapo tarehe hiyo yawe yamehamia kituo hicho.

"Yote hii imeanza baada ya uamuzi wa Rais kuhamishia Makao Makuu Dodoma, na hii miradi ni baadhi tu, ipo miradi mikubwa ambayo utekelezaji wake umeanza ukiwamo ujenzi wa uwanja wa ndege ambao wananchi wamelipwa fidia na fedha zimeshatengwa, lakini uwanja wa zamani umeboreshwa na sasa ndege zinatua hadi usiku," alisema.

Dk. Mahenge pia alisema upo mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara ya mzunguko yenye urefu wa kilometa 110 ambayo mchakato wa ununuzi unakamilishwa ili uanze.

Kiongozi alisema anamshukuru Rais Magufuli kwa kulifanya Jiji la Dodoma kuwa la kisasa.

# TCRA yavionya vyombo vya habari kuelekea uchaguzi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA), imevitaka vyombo vya habari kufanya kazi kwa weledi na kuzingatia maadili katika kipindi cha uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Kaimu Mkuu wa Ofisi ya (TCRA) Kanda ya Kati, Boniface Latia, alitoa rai hiyo jana wakati wa hafla fupi ya utoaji wa leseni kwa kituo cha redio cha Pasua FM jijini Dodoma.

Latia alisema vyombo hivyo vinatakiwa kujiepusha na upotoshaji wa habari katika uchaguzi huo, ili kutosababisha athari kwa jamii.

"Uzembe kidogo unaweza kuligharimu taifa na jamii kwa ujumla kutokana taarifa iliyoandikwa kwenye gazeti au kutangazwa kwenye redio kwa kupotoshwa, hivyo zingatieni maadili ya kazi yenu," alisema.

Vilevile, alitoa rai kwa watumiaji wa mitandao ya kijamii kuzingatia weledi, taaluma na miiko ya uandishi ili kuwafikishia wananchi taarifa sahihi.

Alisema uhai wa chombo chochote cha habari ni kutafuta habari sahihi kutoka katika vyanzo sahihi ili kuufikishia umma.

Latia alisema mamlaka hiyo ni msimamizi mkuu wa sekta ya mawasiliano nchini ambayo inajumuisha sekta ndogo za simu, intaneti, maudhui, utangazaji na huduma za posta.

Alisema katika kusimamia sekta hizo ndogo, ina wajibu wa kutoa leseni za vyombo vya utangazaji na hutolewa baada ya kufikia vigezo vilivyokubalika kisheria.

Latia alisema Ofisi ya Kanda ya Kati inasimamia mikoa ya Singida, Tabora na Kigoma ambayo ina watoa huduma wapatao 15 kwa redio na 20 kwa upande wa mitandao ya kijamii.

Mkurugenzi wa Pasua FM, Erick Cyprian, aliishukuru mamlaka hiyo kwa kuwaamini na kuwapatia leseni.

"Sisi kama Pasua Media tunashukuru mamlaka kwa kutuamini na kutupatia leseni ya utangazaji na tutahakikisha tunazingatia maudhui ya leseni," alisema.

Cyprian alisema kituo hicho kitaongeza ajira kwa wananchi na kukuza pato la familia na taifa kwa ujumla.



Wachuuzi wa ndizi wakifanya biashara kwenye eneo la mzunguko wa barabara ya Soko Kuu la Majengo, jijini Dodoma jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao, endapo ikitokea ajali kwa vyombo vya moto. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# DC aona fursa mauzo ya ufuta ughaibuni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Mwanahamisi Munkunda, amesema umefika wakati serikali kuanza kusafirisha na kuuza nje ya nchi ufuta, ili kuliongeza taifa fedha za kigeni.

Mkunda aliyasema hayo jana jijini hapa alipozungumzia umuhimu wa mfumo wa uuzaji wa mazao kwa njia ya stakabadhi ghalani.

Alisema Tanzania imekuwa mzalishaji mkubwa wa zao la ufuta kulinganisha na mataifa ambayo yanaonekana kuongoza katika usafirishaji wa zao hilo nje ya nchi.

"Tanzania tunaongoza kwa kuwa 'producer' (mzalishaji), lakini siyo 'exporter' (msafirishaji nje ya nchi) na mataifa ambayo mengine hata hayalimi zao la ufuta kama vile Kenya, 'wana-export' kuliko sisi. Sasa ipo haja ya kutafuta namna ya kusafirisha zao hili nje ili kupata fedha za kigeni," alisema.

Alisema kinachotakiwa katika zao hilo ni kuboreshwa usafishaji na ufungashaji kwa njia bora na za kisasa.

Kiongozi huyo wa wilaya alibainisha kuwa katika kipindi hiki cha mavuno, Bahi imepata tani 400,000 za ufuta, ambazo kama zingesafirishwa na kuuzwa nje ya nchi moja kwa moja, zingekuza uchumi wa eneo hilo na kulipatia taifa fedha za kigeni.

"Nchi ambazo hivi sasa zinaongoza kwa uuzaji nje zao hili ni India ambayo na wao pia wananunua hapa kwetu, Ethiopia pia ambao wao katika uzalishaji wanatufutia na Nigeria, hawa ndiyo wanaongoza kwa sasa katika usafirishaji wa ufuta nje," alifafanua.

Munkunda, akizungumzia mfumo wa uuzaji mazao kwa stakabadhi ghalani, alisema utawasaidia wakulima kunufaika na kilimo chao.

Alisema mfumo huo utawadhibiti walanguzi ambao walikuwa wananunua mazao kwa kujipangia bei na kwa vipimo visivyo sahihi.

"Mfumo huu ndiyo utakaomkomboa mkulima na kunufainika na kilimo chake, kwani mkulima atakuwa na sauti ya kupanga bei sahihi iliyopo sokoni na kutumia vipimo sahihi tofauti na ilivyokuwa awali, ambapo wanunuzi walikuwa wanajipangia bei," alisema.

Akizungumzia hali ya chakula katika wilaya yake, kiongozi huyo alisema kuwa kipo cha kutoa kutokana na wakulima kupata mazao mengi msimu huu wa kilimo.

Vilevile, alibainisha kuwa katika kuhifadhi mazingira, kipindi cha msimu wa mvua, wilaya hiyo imepanda miti takribani 150,000.

"Lakini pia tumeagiza kila kaya ni lazima kupanda miti isiyopungua miwili, ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi," alisema.

# Serikali kutengua sheria posho za madiwani

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

SERIKALI inakusudia kutengua sheria ya malipo ya posho za madiwani, kuanzia sasa ili baada ya Uchaguzi Mkuu ujao, madiwani watakaochaguliwa walipwe posho kutokana na asilimia ya makusanyo ya halmashauri zao.

Akizungumza kwenye kikao maalum cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema kuwa uamuzi huo wa serikali unalenga kuzuia fedha zinazopelekwa na Serikali Kuu kwenye halmashauri kutumika kuwalipa madiwani posho.

"Serikali imeamua kutengua sheria ya posho kwa madiwani na kuelekeza kila halmashauri kuwalipa madiwani wake posho kwa asilimia ya makusanyo yake ya mapato ya ndani," alisema Chalamila.

Alisema mbali na kuzuia fedha za maendeleo kuwalipa madiwani posho, uamuzi huo pia unalenga kuhamasisha madiwani kuongeza kasi ya makusanyo ya ushuru kwenye maeneo yao ili waweze kulipwa vizuri.

Chalamila alisema hatua hiyo pia itasaidia madiwani ambao makusanyo ya halmashauri zao yako juu kulipwa kulingana na jasho lao badala ya ilivyo hivi sasa wanalipwa kwa mujibu wa sheria na kupata kiwango sawa na madiwani walio kwenye halmashauri ambazo makusanyo yake ni madogo.

Alisema kuna baadhi ya halmashauri nchini zinakusanya fedha kidogo na jumla ya fedha zinazolipwa kwa madiwani ni nyingi kuliko makusanyo ya ndani ya halmashauri.

"Kuanzia sasa kila mbuzi atakula kwa urefu wa kamba yake, halmashauri ikikusanya fedha kidogo, mjue kuwa hata ninyi madiwani mtalipwa kidogo, lakini mkiongeza bidii ya kukusanya mapato ndivyo ambavyo mtalipwa vizuri," alisema Chalamila.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Hunter Mwakifuna, alisema ili kuongeza mapato ya halmashauri yake, Baraza la Madiwani limebuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitaanza kuiingizia fedha halmashauri hiyo muda wowote.

Alitaja chanzo kimojawapo cha mapato kilichobuniwa na baraza lake kuwa ni maegesho ya magari ambayo wamejenga katika Kata ya Ikimba kwa ajili ya kulaza magari yanayosafiri kwenda nchi za kusini mwa Afrika.

"Maegesho yale tuliyojenga yatusaidia kupata fedha za ushuru wa kulaza magari, lakini hata vijana wetu nao watapata ajira ya kuyalinda magari hayo, tunadhani hiki kitakuwa ni chanzo kizuri cha mapato kwenye halmashauri yetu," alisema Mwakifuna.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Mwajabu Nyamkola, alielekeza utaratibu wa kukamilisha malipo ya madeni ya madiwani ambao wamekopa benki kabla ya kuvunjwa kwa baraza hilo.

Alisema madiwani wote wenye madeni watalipiwa madeni hayo kwa malipo ya miezi 360 ambayo ni sawa na miaka mitano ya utumishi wao na kwamba endapo kuna diwani mwenye deni kubwa zaidi ya fedha itakayotolewa kwa muda huo, itabidi aangalie mwenyewe namna ya kumalizana na benki husika.

Alimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kukamilisha malipo ya madeni ya madiwani hao kabla ya baraza hilo kuvunjwa kisheria ili kusiwapo na malalamiko kutoka kwa madiwani.

Tayari serikali imeelekeza mabaraza ya madiwani nchini yavunjwe kabla ya Juni 10, mwaka huu ili kutoa muda wa Rais kuvunja Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni 19, mwaka huu.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akishuka kwenye boti katika moja ya fukwe za Ziwa Nyasa, wilayani Kyela akiwa katika ziara ya kukagua fursa za uwekezaji zilizopo kwenye fukwe hizo hivi karibuni, ili kuhamasisha wawekezaji. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wananchi waomba wadau kukamilisha kituo afya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANANCHI wa vijiji vitatu vya Kata ya Ilungu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameomba serikali na wadau wengine wa maendeleo kuwasaidia kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya walichoanza kujenga kwa nguvu zao ili kuwaepusha na madhira ya kusafiri umbali wa zaidi ya kilometa 80 kufuata huduma za afya katika hospitali teule ya Wilaya ya Ifisi.

Wananchi hao wanaotoka vijiji vya Shango, Mwela na Kikondo, waliamua kuanza ujenzi wa kituo cha afya katika Kijiji cha Shango, kutokana na kupata shida ya huduma za afya hasa wajawazito na watoto.

Wakizungumza na Nipashe jana, walisema wanaomba wadau na serikali kuwaunga mkono kukamilisha kituo hicho ili waweze kuondokana adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya.

Mwansele Bhilagu wa Kijiji cha Shango, alisema vijana ambao ni nguvu kazi walijitahidi kujitoa kujenga jengo hilo kwa kufyatua matofali na kupasua mbao.

Alisema kutokamilika kwa ujenzi wa kituo cha afya, kunasababisha waendelee kupata adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu katika Hospitali ya Ikonda, wilayani Makete kilometa 200.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Shango, Petro Mwala, alisema, pia wanatoa michango ya fedha na mali zao kwa ajili ya ujenzi na sasa wanahitaji msaada wa kumalizia ujenzi huo.

"Tunahitaji nguvu ya wadau na serikali kukamilisha ujenzi huu tulipofikia panatia matumaini tumejitahidi sana kinamama walikesha kubeba matofali, vijana nao walisaidia sasa kilichobaki ni umaliziaji," alisema Mwala.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kijiji cha Shango, Emily Mwakalila, alisema hadi sasa wananchi hao wameshatumia zaidi ya Sh. milioni 150 kujenga kituo hicho cha afya na kufikia hatua ya kukiezeka na sasa wanahitaji fedha kwa ajili ya umaliziaji.

# Wachimbaji wapongezwa tahadhari corona

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

MKUU wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, amewapongeza wananchi kwa kuendelea kuchukua tahadhari za kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19 hasa kwa wanaondelea na shughuli za uchimbaji madini ya dhahabu.

Mahundi aliyasema hayo jana wakati akipokea vifaa vya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona ikiwamo vitakasa mikono vilivyotolewa na umoja wa madereva wa wilaya hiyo.

Alisema, kwa kushirikiana na viongozi mbalimbali wanaendelea kuchukua hatua muhimu za kukabiliana na maambukizo ya virusi vya corona ikiwamo kufuata maelekezo yanayotolewa na serikali na vifaa hivyo vitapelekwa kwenye maeneo ya kutolea huduma za afya kwa ajili ya watumishi.

"Tunaushukuru umoja wa madereva kwa kuthamini afya za wenzao waliamua kujichanga kwa kidogo wanachokipata na kutukabidhi katoni mbili za vitakasa mikono sabuni chupa 12 kwa ajili ya kunawa mikono vifaa hivi vitagawiwa kwa wahudumu wa afya," alisema Mahundi.

Gwamaka Boniface, miongoni mwa madereva waliokabidhi msaada huo, alisema kutokana na ukubwa wa janga hilo, waliamua kujichanga fedha ili visaidie kuongeza nguvu katika mapambano hayo.

Mkurugenzi wa halmashauri ya wilaya hiyo, Sophia Kumbuli, aliwapongeza wadau waliojitokeza kuchangia vifaa hivyo na kueleza kuwa milango ipo wazi kwa wadau wengine wenye nia kama hiyo.

Alisema wana imani Chunya ni salama dhidi ya ugonjwa wa corona na kuwakaribisha wadau na wawekezaji kwenda kuwekeza kwenye hoteli na huduma nyingine kama benki kwa kuwa mji huo ni wa kibiashara hasa ya madini ambayo inaongeza pato kubwa kwa wilaya.

**Tunaushukuru umoja wa madereva kwa kuthamini afya za wenzao waliamua kujichanga kwa kidogo wanachokipata na kutukabidhi katoni mbili za vitakasa mikono sabuni chupa 12 kwa ajili ya kunawa mikono vifaa hivi vitagawiwa kwa wahudumu wa afya,**





# SMZ yaihakikishia ushirikiano THBUB

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR imesema Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania (THBUB) ina wajibu wa kufanya kazi kwa karibu zaidi na Serikali ya Zanzibar pale inapotekeleza majukumu yake, kwa lengo la kuwatumikia vyema wananchi wa pande zote mbili za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, alisema kuwa kufanya hivyo kutaisaidia serikali kupata nguvu na uwezo wa ziada wa kutatua changamoto zinazowakabili wananchi hususan wanawake, watoto na hata wananchi wenye mahitaji maalum.

Balozi Iddi aliyasema hayo wakati wa mazungumzo yake na uongozi wa juu wa tume hiyo ukiongozwa na Mwenyekiti wake, Jaji mstaafu Mathew Pauwa Mhina, ulipomtembelea ofisini kwake Mjini Zanzibar.

Alisema Tume ina kazi kubwa katika kutekeleza majukumu yake kwa upande wa Zanzibar kutokana na migogoro na changamoto nyingi zinazowakabili wananchi, hali inayosababisha mitafaruku na mifarakano miongoni mwa jamii.

Alieleza kwamba yapo matatizo mengi yanayowakabili wananchi hasa wanawake ya kupewa ovyo talaka na matokeo yake kutelekezwa kunakokwenda sambamba na kuachiwa watoto bila huduma.

Alisema tabia hiyo iliyoanza kuota mizizi kwa baadhi ya wanaume wasiojali utu wa binadamu ni ya hatari kwa mtoto kwa vile inawakosesha haki zao za msingi.

Balozi Iddi alieleza kwamba hivi sasa udhalilishaji wa wanawake na watoto ni janga linaloikumba dunia, hivyo watendaji na viongozi wa Tume lazima wajikite zaidi kushirikiana na vyombo vya dola pamoja na wananchi katika vita vya kukabiliana na tatizo hilo linalochangia mmomonyoko wa maadili ya jamii.

Aliuomba uongozi huo kuandaa mpango maalum wa kujenga majengo ya kudumu ya Ofisi zake Visiwani Zanzibar, na kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko tayari kutoa maeneo ya ujenzi huo wakati wowote pale itapohitajika kutekelezwa mpango huo.

Balozi Iddi alieleza kwamba uwapo wa huduma za ofisi na majengo visiwani Zanzibar mbali ya kuendeleza dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, lakini mfumo huo utawarahisishia watendaji wa Tume hiyo kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Naye Jaji mstaafu Mhina alisema taasisi hiyo ni chombo cha umma kilichoundwa kusimamia upatikanaji wa haki za binadamu ili kusimamia utawala bora nchini.

Hata hivyo, alisema watendaji wa Tume hiyo ni binadamu wanaoweza kutekeleza katika utekelezaji wa majukumu yao, hivyo viongozi wakuu wanapaswa kushauri pale watendaji hao wanapotekeleza katika maeneo yao ya kazi.

Aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kazi kubwa na ngumu inayofanya ya kuhudumia wananchi, jambo ambalo uongozi wa tume hiyo unaliunga mkono.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, akizungumza na wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Zanzibar, alipofanya ziara ya kutembelea chuo hicho baada ya vyuo kufunguliwa..**PICHA|: RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR**

# Wanavyuo, wanafunzi waaswa corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wanafunzi ambao wameanza vyuo na wa kidato cha sita kujitahidi kufuata masharti yaliyotolewa na wataalamu wa afya katika kujikinga na corona.

Akizungumza na wanafunzi hao wakati alipofanya ziara ya kuangalia namna maagizo yaliyotolewa yanavyotekelezwa katika Chuo cha Kiislamu Mazizini, alisema corona ni hatari, hivyo ni vyema kwa wanafunzi kufuata maelekezo yanayotolewa kwa ajili ya kujikinga wao na familia zao.

Pembe alisema ugonjwa huo umeikumba dunia nzima, hivyo ipo haja ya kuyafanyia kazi maelekezo yanayotolewa ili kuutokomeza kabisa.

Aidha, alielezea kuridhishwa na namna uongozi wa chuo hicho ulivyofuata maagizo yaliyotolewa pamoja na wanafunzi wao na kuwataka kuendelea pamoja na kuongeza juhudi katika masomo, ili kuweza kufaulu vizuri na kupata walimu bora na wataalamu.

Mkuu wa Taaluma wa Chuo hicho, Mohammed Mwinyi Ramadhan, alisema wamefarajika kuona serikali imeweka mipango madhubuti na kuhakikisha wanarejesha huduma za utoaji wa elimu.

Mkuu huyo aliahidi kuendelea kuyafanyia kazi maelekezo yote yanayotolewa na serikali pamoja na wataalamu wa afya.

Wanafunzi wa chuo hicho walielezea kufurahishwa kwao pamoja na kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuandaa miundombinu mbadala kwa wanafunzi ili kuhakikisha shughuli za masomo zinarejea kama kawaida.

# Wawakilishi wahoji usajili meli za kigeni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuifuatilia Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar (ZMA) ambayo imesitisha kufanya usajili wa meli za kigeni.

Wamesema hali hiyo inaiathiri mamlaka hiyo kwa kukosa fedha za kujiendesha.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Mwakilishi wa Jimbo la Paje, Jaku Hashim Ayoub, alisema huu ni mwaka wa tatu sasa tangu mamlaka isitishe usajili wa meli za kigeni baada ya kubainika meli zilizopewa kibali baadhi yake kusafirisha dawa za kulevya.

Alisema suala hilo linazungumzika ambapo serikali inatakiwa kufuatilia na kujua hatima ya mamlaka kuhusu kurejea tena kufanya kazi hiyo kwa mujibu wa sheria.

"Mheshimiwa Spika, tumesikitishwa hadi sasa mamlaka imeshindwa kutekeleza majukumu yake ya kusajili meli za kigeni za mizigo, baada ya kutakiwa kusitisha zoezi hilo kufuatia meli zilizopewa usajili kubainika kusafirisha dawa za kulevya," alisema.

Alieleza kuwa mamlaka kwa sasa inakabiliwa na hali ngumu ya kujiendesha ambapo imelazimika kutafuta fedha kwa kutoza kodi kwa vyombo vya usafiri vya kawaida ikiwamo boti za uvuvi.

"Mamlaka kwa sasa inakabiliwa na hali ngumu ya uendeshaji kiasi kulazimika kukusanya mapato na kutoza kodi kwa vyombo vya kawaida ikiwamo majahazi kwa sababu usajili waliokuwa wakiufanya wamepigwa marufuku kufanya hivyo," alisema.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, alisema suala la mamlaka hiyo kusitishwa kufanya kazi za usajili wa meli za kigeni linazungumzika na pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Suala hili linazungumzika na wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kuweka njia mbadala ambazo litaiwezesha mamlaka kufanya shughuli zake kwa mujibu wa sheria," alisema.

Mamlaka ya Usafiri Baharini ya Zanzibar (ZMA) kwa zaidi ya miaka mitatu sasa imesitisha kufanya shughuli za usajili wa meli za kigeni baada ya kubainika meli hizo kujishughulisha na biashara ya dawa za kulevya, huku zikiwa zinapeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano.

Akitoa ufafanuzi wa hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia suala la Mamlaka ya Usafiri Baharini ya Zanzibar kusitisha kazi ya kusajili meli za kigeni na kupeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Sira Ubwa Mamboya, alisema serikali ipo katika mchakato wa kufanya marekebisho ya sheria ya mamlaka hiyo ili kuongeza ufanisi wa majukumu yake.

"Ni kweli Serikali ya Jamhuri ya Muungano imetoa agizo la kuitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Baharini kwa sasa kuacha kufanya usajili wa meli za kigeni zinazopeperusha bendera ya Tanzania kutokana na baadhi yake kubainika kujishughulisha na kusafirisha dawa za kulevya," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Yassin Bakar Swai** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba ya usajili **T332 AQZ** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi taarifa:

**DAR/GOG/RB/179410/2020**

115762902

## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**JS GROUP COMPANY LIMITED** ana tangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 275 CBL.** Aina yake **HAUJOE.** Yenye chassis namba **LC6PCJK27JOO55276** na injini namba **156FM15AD2F43158.**Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi:

**MOR/MOR/RB/254078/2020.**

115763502

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA IRAMBA**

**MAHALI KIOMBOI-BOMANI**

**MAOMBI NA.13 MWAKA 2020**

**MARIAMU MOHAMED.........................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ELIZABETH NEHEMIA.........................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA; ELIZABETH NEHEMIA**
**WA IBAGA**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/ tarehe 30 mwezi 06 mwaka 2020 saa 2.00 Asubuhi mbele ya Mh. B.J Shuma mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
**AMIRI** hii imetolewa kwa mkono wanguna Lakiri/Muhuri wa Baraza hili la Tarehe 28 mwezi wa 05 mwaka 2020.

**UTHUBITISHO WA KUPOKEA**
**Mimi ..............................**
**Nimepokea Wito/Kuitwa Shauri**
**Saini....................................**
**Tarehe.................................**

MWENYEKITI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 45/2020**

**Ombi la CHRISTINA JOHN KUPAZA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu MICCAH SONGELAEL SETH**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 22/6/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 03/6/2020.

115762202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;112/2020**

**Ombi la MARIAM OMARY Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SIJAONA SALUM MAGATI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 28/05/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe ____/20__

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115762102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;124/2020**

**Ombi la SARAH SHAHA MUSSA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ASIA SHAHA MUSSA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 09/06/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 19/05/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115762502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;103/2020**

**Ombi la HASSAN CHUMA KILAMA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MNGOMA ABDU KILAMA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/06/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 18/05/2020.

Tarehe 15/5/2020

HAKIMU

115762702

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FOMU II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 133/2020**

**Ombi la GOTFRIED FELIX MAPUNDA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu STEVEN GEORGE MAPUNDA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 02/07/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 02/06/2020.

Tarehe 2/6/2020

HAKIMU

115763002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;140/2020**

**Ombi la ATHUMAN SAID BAKARI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MAUA HUSENI MWISHEHE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/06/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/06/2020.

Tarehe 4/6/2020

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115763602


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati ye na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Obama awasifu vijana wanaoandamana

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa zamani wa Marekani, Barack Obama, alisema kuwa anaamini Marekani itakuwa bora zaidi kutokana na kuwa vijana wako kwenye mstari wa mbele kushinikiza mabadiliko kupitia maandamano yanayoendelea nchini humo.

Katika hotuba yake ya kwanza tangu kuuawa kwa Mmarekani mweusi, George Floyd, katika mazingira yaliyoibua utata na mjadala mkubwa wa kitaifa, Rais Obama alisema kuna tofauti kubwa kati ya sasa na miaka ya 60.

Alisema miaka iliyopita harakati za kutetea haki za wachache katika jamii, hazikutekelezwa na watu wa tabaka mbalimbali kama ilivyo leo.

"Nimesikia baadhi ya watu wakisema msukumo huu unaoendelea sasa unawakumbusha miaka ya sitini. Lakini ukiangalia sasa, kuna tofauti," alisema mwanasiasa huyo.

Obama alisema hayo wakati wa mkutano kwa njia ya mtandao uliofadhiliwa na shirika la Obama Foundation.

Bila kutaja jina la yeyote, Obama alisema kuwa ni wakati wa kushinikiza walioko madarakani kuchukua hatua.

Obama alisema kuwa ni wakati wa kufahamu kuwa maisha na ndoto za wale wanaojihisi wanalengwa yanathamani.

"Ni wakati wa kila mmoja kutembea anakotaka bila kuwa na wasiwasi wa kushambuliwa," alisema Obama.

Aliongeza kuwa jukumu kubwa liko kwa walinda sheria kwa kuwa watu wengi wamegadhabishwa na tabia za baadhi ya maofisa wa polisi.

Hata hivyo alisema kuwa polisi wengi wanatekeleza jukumu lao ipasavyo na kwamba wanakaribiswa kwenye mjadala unaoendelea.

***VOA***



Raia wa Marekani wakiwa wamekusanyika wakati wa maandamano ya kupinga vitendo vya ubaguzi wa rangi baada ya kutokea kifo cha George Floyd.**PICHA:REUTERS**

# Maofisa wengine watatu wajumuishwa kesi Flyod

**WASHINGTON, Marekani**

MWENDESHA mashtaka mkuu wa Jimbo la Minnesota nchini Marekani ameongeza uzito wa mashtaka dhidi ya afisa wa polisi aliyemkaba koo kwa goti lake, George Floyd, Mmarekani mweusi aliyekufa akiwa mikononi mwa polisi.

Mashtaka dhidi ya mtuhumiwa mkuu katika kifo hicho cha George Floyd , aliyekuwa ofisa wa polisi, Derek Chauvin, yamepandishwa kutoka mauaji ya daraja la tatu ambayo siyo ya kukusudia, hadi daraja la pili ambalo linahusisha dhamira ya kuuwa, au mauaji yaliyosababishwa na uzembe na kutojali.

Adhabu ya mauaji ya aina hiyo nchini Marekani inaweza kufikia miaka 40 jela.

Maofisa wengine watatu waliokuwa pamoja na Derek Chauvin pia wamekamatwa na kufunguliwa mashtaka. Wawili miongoni mwao walionekana kumkanyaga mgongoni marehemu Floyd wakati Chauvin alipokuwa amemkaba koo, na mwingine alisimama kando akitazama tu bila kufanya chochote.

Mwendesha mashtaka mkuu wa jimbo la Minnesota, Keith Ellison, alisema kumtia hatiani ofisa wa polisi nchini Marekani ni mchakato mgumu sana, ambao unachukua muda mrefu, na kusikitika kuwa hali hiyo imeharibu imani ya umma kwa mfumo wa sheria.

"Nitakuwa mkweli hapa, kesi za aina hii hazikupewa uzito jimboni Minnesota na nchini kote Marekani, na nadhani kuporomoka kwa imani kumetokana na historia ndefu ya kukosa utashi wa kuwawajibisha wale wenye majukumu ya kusimamia uwajibikaji katika jamii," alisema Ellison.

Kifo cha George Floyd na mazingira yake viligusa hisia za watu kote ulimwenguni, na kuzusha maandamano ambayo wakati mwingine yamekumbwa na ghasia na uporaji.

***DW***

## Kenya yahamishia uchukuzi wa mizigo Naivasha

**NAIROBI, Kenya**

KENYA imeanza kuhamisha operesheni za kuchukua makasha ya mizigo kutokea mjini Mombasa hadi bandari kavu iliyoko Naivasha, ili kupunguza safari za malori ya mizigo kutoka nchi za Uganda, Rwanda na Sudan Kusini.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na Waziri wa Uchukuzi wa Kenya, James Macharia, hatua hiyo imeambatana na agizo la viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki la kuzuwia virusi vya corona kusambaa wakati madereva wa malori wanasafirisha bidhaa.

Waziri Macharia alisema manufaa ni mengi zaidi kwa wafanyabiashara hao kupokea mizigo yao kutokea Naivasa badala ya bandarini Mombasa.

Bandari ya nchi kavu ya Naivasha inasadikika kuwa na vifaa vinavyohitajika kama vilivyoko Mombasa kurahisisha shughuli ya kusafirisha mizigo.

Alisema mbali ya kuwako nafasi ya kutengeneza ofisi za muda kwa kampuni husika, makasha matupu yatasafirishwa moja kwa moja hadi Mombasa bila malipo ya ziada.

Alisema hakuna malipo ya ziada baada ya kupokea mizigo kwenye bandari ya nchi kavu ya Naivasha na kwa sasa wafanyabiashara hawatozwi chochote kuhifadhi makasha yao kwenye mabohari hayo.

Takwimu za Wizara ya Uchukuzi ya Kenya, zimeonesha kuwa mfanyabiashara atahitaji kati ya dola 1,930 na 2,180 kusafirisha kasha la futi 20 na 40.

Alisema kuna mipango ya kuifufua reli inayoziunganisha Mombasa na Malaba iliyoko mpakani.

**DW**

# Rais Trump adaiwa kuwagawa Wamarekani

**WASHINGTON, Marekani**

ALIYEKUWA Waziri wa Ulinzi wa Marekani, James Mattis, amemshutumu Rais Donald Trump, kwa kuleta mgawanyiko na kutumia vibaya mamlaka yake.

Katika maoni aliyotoa, Mattis alisema Rais Trump ameamua kugawanya watu wa Marekani na pia ameshindwa kuonesha uongozi uliokomaa.

Alisema alikasirishwa na kufadhaishwa sana na namna Rais Trump alivyoshughulikia maandamano yanayoendelea nchini humo.

Mattis alijiuzulu mwaka 2018 baada ya Rais Trump kuamua kuondoa majeshi ya Marekani kutoka Syria.

Tangu wakati huo amekuwa kimya hadi utawala wa Rais Trump ulipokosolewa vikali katika gazeti la Atlanta Jumatano.

Baada ya kumkosoa, Rais Trump alituma mfululizo wa ujumbe kwenye mtandao wa Twitter ambapo alisema Mattis alisemekana kuwa ofisa wa thamani ya juu zaidi duniani.

"Sikupenda mtindo wake wa uongozi au yeye mwenyewe na wengine wengi wanakubaliana na hilo, Rais Donald Trump ndiyo rais wa kwanza kwa maisha yangu ambaye hawaunganishi raia wa Marekani, hata hajifanyi pengine anajitahidi katika hilo,badala yake, anajitahidi kutugawanya," aliandika Mattis katika gazeti la The Atlantic. "

Aliendelea kusema kuwa: "Tunashuhudia miaka mitatu ya hatua hizi za kukusudiwa. Tunashuhudia matokeo ya miaka mitatu ya uongozi ambao haujakomaa".

Mattis pia alizungumzia wimbi la hivi sasa la maandamano dhidi ya ubaguzi wa rangi ambako kuchochewa na kifo cha raia Mmarekani mweusi, George Floyd, aliyekufa mikononi mwa polisi mapema mwezi huu.

Maofisa wanne wameshtakiwa kuhusiana na kifo cha Floyd kilichotokea Minneapolis Mei 25.

"Maandamano haya yanafafanuliwa na dhamira ya maelfu ya watu ambao wanasisitiza kwamba tuishi kulingana na maadili yetu... kama taifa, Hatustahili kutatizwa na wachache ambao ni wavunjaji wa sheria," alisema Mattis.

Ofisa huyo aliyestaafu, ambaye alijiuzulu Desemba, 2018 alikosoa vikali sera ya kigeni ya Rais Trump na pia akashutumu utumiaji wa jeshi kama njia ya kujibu maandamano yanayotokea.

"Sikuwahi kufikiria kwamba jeshi... litaamrishwa kwa chochote kile kitakachotokea kukiuka haki ya kikatiba kwa raia wake wenyewe, kufanya wanajeshi kama njia ya kutatua hili, kama ilivyoshuhudiwa Washington DC, kunasababisha mgogoro... kati ya jeshi na raia," alisema Mattis.

***BBC***

## HABARI MICHEZO



# KROOS AJIPA MATUMAINI KWA REAL MADRID

**MADRID, Hispania**

KIUNGO wa Real Madrid, Toni Kroos, anaamini timu yake itazoea haraka mazingira wakati msimu wa LaLiga utakaporejea tena wiki ijayo na kufurahia mafanikio.

Baada ya kusimama tangu Machi, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, kampeni ya LaLiga inatarajia kuendelea tena Juni 11, mwaka huu.

Madrid wapo nyuma kwa pointi mbili dhidi ya vinara ambao ni wapinzani wao, Barcelona huku zikiwa zimesalia mechi 11 kumaliza msimu.

Kroos, ambaye kikosi chake kitaanza dhidi ya Eibark, amesema yoyote atakayezoea haraka mazingira ya kucheza bila mashabiki atafanikiwa.

"Tunajifua sana ili mchezo wetu wa kwanza uwe bora kadiri itakavyowezekana. Hatuwezi kufanya zaidi, hali ipo sawa tu kwa kila mmoja," amesema akiiambia televisheni ya Real Madrid.

"Tunatakiwa kujifua vizuri ili kurudi kwenye 'ufiti' wetu, tunatakiwa kucheza kwa kuzoea haraka mazingira ya kuwapo uwanjani bila mashabiki, na mechi 11 zilizobaki zinaweza kutupa mafanikio.

"Hii ni mara ya kwanza tunacheza mechi bila mashabiki wetu uwanjani, ngoja tutaona nini kitakachotokea, na timu itakay-

## LEVERKUSEN YAJIPANGA KUMBAKISHA KAI

**MUNICH, Ujerumani**

KAI Havertz atajiunga na "klabu ya daraja la duniani" kwa siku za usoni, lakini Rudi Voller ana matumaini ya kumbakisha pale Bayer Leverkusen kwa mwaka mwingine.

Fowadi huyo wa Leverkusen, Havertz, amekuwa akihusishwa sana na Bayern Munich, Manchester United, Liverpool na Real Madrid lakini Kocha Mkuu, Peter Bosz alisema Machi kwamba ana thamani ya angalau euro milioni 100.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 alifunga mabao 17 kwenye Bundesliga msimu wa 2018/19 na msimu huu amefunga mara 11 na kutoa pasi za mwisho tano katika mechi 26 alizocheza kwenye mashindano yote.

Mkurugenzi wa Michezo wa Leverkusen, Voller anatambua kwamba ni suala la muda tu hadi Havertz aondoke hapo kwenye dimba la BayArena kwenda kwenye vitu vikubwa.

Hata hivyo, ana matumaini atafanikiwa kumshawishi mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani kuendelea kuwa hapo angalau kwa msimu mmoja zaidi.

"Anajisikia vizuri na huru, bado ana mkataba hadi 2022, lakini tunajua kwamba Kai atakwenda kwenye klabu ya daraja la juu," amesema Voller akiiambia Sky Sports.

"Lakini bado yupo hapa, na bado nina matumaini kuendelea kumbakisha hapa kwa angalau mwaka mmoja na nina uwezo wa kufanya hivyo."

# PSG yaivunja nguvu Barca kwa Neymar

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain inataka euro milioni 175 ili kumwachia Neymar anayetakiwa kwa udi na uvumba na Barcelona, kwa mujibu wa Sport.

Neymar aliondoka Barca kwenda PSG kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222 kwenye soko la usajili mwaka 2017, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Brazil ameendelea kuhusishwa na kurudi Camp Nou.

Lakini sasa matumaini ya Barca kumaliza dili hilo yapo shakani kutokana na kiasi kikubwa cha fedha wanachokitaka PSG pamoja na janga la mlipuko wa virusi vya corona na pia mpango wao wa kumtaka fowadi wa Inter Milan, Lautaro Martinez.

Kutua kwa Martinez na Neymar pale Barca mwishoni wa msimu huu ilikuwa ni ndoto kubwa ya miamba hao wa Katalunya.

Nia yao ilikuwa kuunda safu ya ushambuliaji yenye nguvu kwa kutengeneza upatina kati ya Martinez na Neymar.

Lakini sasa ni wazi kwamba, mpango wa Barca kumsajili Neymar unaweza kuota mbaya kutokana na matatizo ya kifedha yanayoikabili timu hiyo kutokana na corona.



# MARADONA

## ASAINI MKATABA MPYA NA GIMNASIA

**BUENOS AIRES, Argentina**

DIEGO Maradona amemaliza uvumi ulioenea juu ya majaliwa yake baada ya kusaini mkataba wa mwaka mmoja na klabu Gimnasia ya Esgrima La Plata ya nchini Argentina.

Gwiji huyo wa Argentina aliteuliwa kuwa kocha mkuu wa Gimnasia Septemba, mwaka jana, ingawa aliondoka kwa muda mfupi Novemba na alirudi siku mbili baadaye.

Maradona mkataba wake ulimalizika mwishoni mwa msimu huu na ilionekana walishindwa kufikia makubaliano mwanzoni mwa wiki hii.

Hata hivyo, Gimnasia, wakati wanasheherekea kutimiza miaka 133 tangu kuanzishwa kwake Jumatano, ilithibitisha kwamba wamemwongezea mkataba Maradona hadi mwaka 2021.

Klabu hiyo iliweka ujumbe kwenye ukurasa wake wa Twitter uliosomeka: "Unajulikana kama Pelusa, Barrilete Cosmico, Mungu, Diego, Diegote, nahodha...

"Kwa upande wetu, wewe ni zaidi ya Tripero na moyo wako tayari una rangi zetu za bluu na nyeupe."

Maradona awali alidokeza kufikia makubaliano na aliwapongeza Gimnasia kwa kumbukizi yao hiyo kupitia kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Leo ni siku ya kumbukumbu ya kuzaliwa El Lobo," aliandika. "Hongereni @Gimnasia_Oficial pamoja na mashabiki wenu!!!

"Moyo wangu ni wa rangi ya bluu na nyeupe. Haya twende zaidi!!!"

Ligi Kuu Argentina, Primera ilimalizika Aprili, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, huku timu za kushuka daraja zimeahirishwa kwa miaka miwili.

Gimnasia walikuwa nafasi ya 19 katika timu 24 wakati msimu ukifungwa.

# Heskey afurahia Liverpool kusubiria taji la EPL

**LIVERPOOL, England**

EMILE Heskey anaamini kusubiriwa kwa Liverpool kushinda taji la Ligi Kuu England "ni jambo la kupendeza kwenye soka".

Kikosi hicho cha Kocha, Jurgen Klopp kinaongoza msimamo wa ligi hiyo kwa pointi 25 mbele ya bingwa mtetezi, Manchester City na sasa wanakaribia kushinda taji hilo kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30.


Taji hilo litakuwa ni la 19 kwa Liverpool, ikiwa imetawala ligi hiyo kuanzia miaka ya 1970 na 1980.

Straika wa zamani wa wekundu hao, Heskey anaamini soka itanufaika kwa moja ya klabu kongwe kuwa juu kwa mara nyingine tena.

"Ni jambo la kupendeza," amesema Heskey akiiambia Stats Perform News.

"Ni klabu kubwa, na huwezi kuthibitisha hilo hadi uende pale, hadi utakapotembea kwenye mitaa ya Liverpool ndo utaona tofauti yake."

"Hili ni jambo kubwa kumaliza kipindi cha miaka 30 kwa Liverpool. Taji la Ligi Kuu England halijabebwa na Liverpool. Na sasa ni wazi huu ndio wakati wake."




# Roma yajiandaa kumsajili Pedro

**LONDON, England**

WINGA Pedro anajiandaa kusajiliwa na Roma kama mchezaji huru baada ya mkataba wake na Chelsea kumalizika mwishoni mwa msimu huu.

Mhispania huyo anakaribia kumaliza muda wake wa kukaa Stamford Bridge mwishoni mwa msimu huu na tayari ameanza mazungumzo na klabu nyingine.

Kwa mujibu wa gazeti la AS Hispania, Pedro anaipa nafasi ya kwanza Roma na taarifa hiyo pia inaandikwa kwenye gazeti lingine la Italia liitwalo Il Tempo, baada ya kukaa kwa muda wa miaka mitano kwenye klabu hiyo ya London Magharibi.

Uamuzi huo umesababishwa na klabu nne kubwa wakiwamo vigogo wa Serie A Juventus, Sevilla, Valencia na Real Betis, linaandika gazeti la Mundo Deportivo.

Roma inaongoza katika mbio za kuwania saini ya winga huyo mwenye umri wa miaka 32, na inaonekana inakaribia kukamilisha mchakato huo.

Pedro alijiunga na Chelsea mwaka 2015 akitokea Barcelona, na ameichezea mechi 201 klabu hiyo ya Ligi Kuu England.

Tangu alipotua Stamford Bridge, Pedro ameshinda taji moja la Ligi Kuu England, Kombe la FA na Ligi ya Europa League mara moja, na anaamini Chelsea itamaliza katika nafasi juu nne kwenye msimamo wa ligi hiyo kabla ya kuondoka.

Katika msimu huu, Mhispania huyo amefunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho tatu kwenye michezo 18 aliyocheza kwenye mashindano mbalimbali akiwa chini ya Frank Lampard.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MULLER AUCHAMBUA UWEZO WA LEWANDOSKI

●●●Aeleza anatamani kucheza pamoja na mshambuliaji huyo kuliko Messi au Ronaldo...

**MUNICH, Ujerumani**

THOMAS Muller amebainisha angependa kucheza pamoja na mchezaji mwenzake wa Bayern Munich, Robert Lewandowski kuliko Lionel Messi au Cristiano Ronaldo.

Muller aliulizwa kama angependa kuwa na Messi au Ronaldo kama mchezaji mwenzake katika kikosi kimoja wakati wa mahojiano ya Jumatano.

Mshambuliaji huyo wa Bayern alibainisha staili yake ya uchezaji itafanya kazi bora zaidi kama akicheza na Ronaldo kuliko Messi, lakini akaongeza Lewandowski ndio yupo juu ya wote.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Ujerumani, Muller ametoa pasi za mwisho 18 kwenye Bundesliga msimu huu, huku Lewandowski amefunga mabao 29 wakati Bayern wakijiweka kwenye nafasi ya kubeba tena taji.

Hata hivyo, mshindi huyo wa Kombe la Dunia anawatambua Messi na Ronaldo kama wachezaji wa daraja la juu kabisa na hawezi kuwalinganisha na wachezaji wengine.

"Pengine kwa kipindi kilichopita ningependa kucheza na Leo Messi, kwa sababu kwa miaka sita au saba ya mwanzo wakati naanza kucheza, nilikuwa mshambuliaji wa kupokea zaidi mipira," amesema Muller.

"Nilikuwa napewa mpira ndani ya 'box' na kujaribu kufunga. Lakini kwa sasa nipo katika wakati tofauti na mimi ninatoa zaidi pasi za mwisho za kufunga mabao.

"Pengine kwa sasa namhitaji zaidi Cristiano Ronaldo kufunga mabao, lakini sisi pale Bayern tuna Robert 'Lewan-goal-ski'! Nafikiri kwa sasa yeye ni bora zaidi kucheza nae kuliko Cristiano.

"Nimecheza dhidi yao wote wawili (Messi na Ronaldo), nimeshinda dhidi yao wote wawili na nimepoteza dhidi yao wote wawili."

## KWA UFUPI

**MADRID YAMTAKA SANCHO**

REAL Madrid imeweka wazi inataka kumsajili winga wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, ambaye ana umri wa miaka 20. ***(AS)***

**DEMBELE ATAKIWA BARCA**

JUVENTUS imeanza mazungumzo na Barcelona kwa ajili ya kumsajili kwa mkopo kiungo mshambuliaji Mfaransa Ousmane Dembele, ambaye ana umri wa miaka 23 katika majira ya joto. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**SANCHEZ, SMALLING KUUZWA**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anatarajia kutunisha mfuko wa fedha wa klabu kwa kuwauza nyota wake akiwamo beki, Marcos Rojo (30), beki wa kati, Chris Smalling (30) na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Chile, Alexis Sanchez (31). Klabu imeyumba kwa sababu ya janga la corona. ***(Evening Standard)***

**ROJO KUREJEA UNITED**

BEKI Marcon Rojo anajiandaa kurejea Manchester United baada ya Kocha wa Estudiantes, Leandro Desabato, kukiri beki huyo anaonekana kumaliza mkataba wake wa mkopo. ***(FM Radio Late 93.1 via Mail)***

**FRASER KITAELEWEKA**

NYOTA wa Bournemouth, Ryan Fraser (26), ambaye anajiandaa kuondoka katika klabu hiyo akiwa mchezaji huru ifikapo majira ya joto, anatajwa huenda akawa mmoja wa wachezaji ghali kwenye Ligi Kuu England hivi karibuni. ***(The Athletic - subscription only)***

**PSG KUIKAMUA BARCA**

MABOSI wa Paris St-Germain wanahitaji kulipwa pauni milioni 156 taslimu na Barcelona ili kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Neymar ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Sport - in Spanish)***

**EPL KUREJEA TOFAUTI**

MASHABIKI wanatarajia kupata fursa ya kusikia sauti 'feki' za mashabiki wakati mechi za Ligi Kuu England zitakaporejea. ***(Mirror)***

**BURGOS KUONDOKA ATLETICO**

MJERUMANI 'Mono' Burgos (51), amethibitisha ataondoka katika nafasi yake ya Kocha Msaidizi kwenye klabu ya Atletico Madrid mwishoni mwa msimu na kuhitaji kujiendeleza kwa kuajiriwa kama Kocha Mkuu. ***(Marca)***

**MARADONA MAMBO SAFI**

MCHEZAJI mkongwe wa Argentina, Diego Maradona (59), ataendelea kuwa Kocha wa klabu ya Gimnasia y Esgrima ya nchini humo mwaka mwisho wa msimu wa 2020/21 baada ya kuongeza mkataba mpya. ***(Reuters)***

**MARSCH ATAJWA DORTMUND**

KOCHA Jesse Marsch (46), wa Red Bull Salzburg ambaye ni raia wa Marekani anatajwa huenda akarithi mikoba ya Lucien Favre kwenye kikosi cha Borussia Dortmund. ***(Bild - in German)***

**ROBERTO ANUKIA CITY**

MANCHESTER City inajiandaa kumsajili Sergi Roberto kutoka Barcelona, lakini inaelezwa uhamisho wa mshambuliaji huyo hautakuwa wa moja kwa moja. ***(Mundo Deportivo)***

**UNITED YAMGANDA MADDISON**

MABOSI wa Manchester United bado wanajipanga kuwania saini ya kiungo wa Leicester City, James Maddison, lakini inaelezwa vigogo hao wanatakiwa kuanza upya mazungumzo ya mchakato huo. ***(Daily Mail)***

HABARI MICHEZO

# AZAM YAANZA 'KUITISHA' SIMBA MICHUANO YA FA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC umesema hauna mashaka ya aina yoyote juu ya mchezo wao wa hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Simba unaotarajiwa kufanyika kati ya Juni 27 na 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema hawatauchukulia rahisi mchezo huo na wanajipanga kupambana ili kupata ushindi na kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Popat alisema hawana hofu na Simba kwa sababu wana kikosi imara na wanafahamu umuhimu wa mchezo huo ambao unasubiriwa kwa hamu na mashabiki wa timu zote mbili.

Alisema tayari wameshafanya kikao cha Kocha Mkuu, Aristica Cioaba baada ya kuwasili nchini kwa ajili ya kuanza mipango ya kusaka ushindi katika mchezo huo na michezo 10 Ligi Kuu Tanzania Bara iliyobakia.

"Ni ngumu kusema kama hatupo tayari ilhali kikosi chetu kipo vizuri na ni mabingwa watetezi, hatuna mashaka na dakika 90 huwa hazidanganyi, tutapambana kusaka matokeo, tunawaheshimu wapinzani wetu na pia hii ni mechi ya kisasi kwetu, tunahitaji ushindi," alisema Popat.

Kiongozi huyo alisema malengo yao ni kutetea ubingwa wanaoushikilia na watashirikiana 'bega kwa bega' na benchi la ufundi, ili malengo hayo ya kutetea taji hilo ambalo ndio tiketi ya kushiriki katika michuano ya kimataifa.

"Tunachoangalia kwa sasa ni mpinzani wetu ambaye tunakutana naye katika hatua ya robo fainali ambaye ni Simba, ni mchezo mgumu na wa kisasi, kwa sababu hatutakuwa tayari kuona wanatufunga kwa mara nyingine kama ilivyo kwenye ligi," alisema mtendaji huyo.

Azam ndio mabingwa watetezi wa michuano ya Kombe la FA baada ya kuifunga Lipuli FC ya Iringa bao 1-0 katika mchezo wa fainali uliochezwa mkoani Lindi mwaka jana.



Beki wa Simba, Erasto Nyoni (kushoto), akijaribu kumiliki mpira katika mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa kuendelea na kampeni ya kutetea taji la Ligi Kuu Bara. **PICHA: SIMBA SC**

# Ameir apata ulaji Zanzibar

**Na Hawa Abdallah**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limemteua, Ali Ameir kuwa Kaimu Katibu Mkuu wa shirikisho hilo akichukua nafasi ya Mohamed Ali Hilali "Tedy".

Awali Ameir (pichani), alikuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya ZFF.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa ZFF, Seif Kombo Pandu, alisema shirikisho hilo lina imani na Ameir na wanatarajia atafanya majukumu yake vema kwa sababu ya uzoefu aliokuwa nao.

Pandu alisema uteuzi huo umefanyika kwa kufuata katiba ya ZFF ikiwamo kuangalia sifa ya kiongozi kuwa na elimu ya kuanzia ngazi ya shahada.

"Tumemteua Ameir kuwa Kaimu Katibu Mkuu, kwa kifupi atafanya kazi zote za Katibu Mkuu wa ZFF kama ilivyokuwa kwa katibu aliyepita ambaye alifanya majukumu yake kwa umakini," alisema Pandu.

Amewaomba wanachama wa shirikisho hilo kumpa ushirikiano ili kufanikisha safari ya soka la Zanzibar inakwenda vema kama inavyokusudiwa.

Ameir pia ni mfanyakazi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Visiwani Zanzibar.



## Wachezaji Coastal Union 'vibonge'

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union ya jijini Tanga, Juma Mgunda, amesema idadi kubwa ya wachezaji wake wamerudi wakiwa na uzito jambo ambalo 'linamuumiza kichwa', kuelekea hatua ya lala salama.

Mgunda alisema ana kibarua cha kuwarudisha wachezaji hao katika uzito wa kawaida ili kuendelea kufanya vizuri kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zilizobakia.

"Wachezaji wangu wengi wamerudi wakiwa wameongezeka uzito kitu ambacho hakipaswi mchezaji kuwa katika hali hiyo," alisema Mgunda.

Kocha huyo amewataka wachezaji hao kuongeza juhudi katika mazoezi ili wasipoteze nafasi ya kupangwa katika kikosi cha kwanza.

"Sitaki lawama kila anayejua amezidi uzito nimemwambia ajitume la sivyo watakuwa wanakaa benchi kwa sababu watakuwa wepesi uwanjani," alisema Mgunda.

Aliongeza ukitoa kasoro hiyo, kikosi chake kinaendelea vema na mazoezi na mpaka jana mchana hana majeruhi hata mmoja jambo ambalo anamshukuru Mungu.

"Kwanza ni jambo la kumshukuru Mungu wachezaji wangu wote wamerudi salama, kinachofuata ni kuyafanyia kazi upungufu uliyopo kabla ligi haijaanza," Mgunda alisema.

Coastal Union itaikaribisha Namungo FC Juni 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM, Mkwakwani.

## Kabaddi Afrika kufanyika nchini

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Pili ya mchezo wa Kabaddi Afrika yanatarajiwa kufanyika kuanzia Desemba 11 hadi 13, mwaka huu jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Tayari nchi nane zimeshathibitisha kushiriki mashindano hayo.

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Mwenyekiti wa Kabaddi Tanzania, Abdallah Nyoni, alisema tayari wameshaanza maandalizi kuelekea michuano hiyo.

Nyoni alizitaja nchi zilizothibitisha kuwa ni pamoja na Uganda, Kenya, Cameroon, Misri, Maurtius, Siera Leone, Zimbabwe na wenyeji Tanzania.

"Timu kutoka England, Malaysia, Taiwan na Iraq zimethibitisha kushiriki lakini bado zinasubiri uamuzi kutoka katika vyama vyao, lakini vikishirikiana na mabosi wa dunia kama zitashiriki au laa," alisema Nyoni.

Alisema wanaamini mashindano hayo yatasaidia kutangaza jina la Tanzania na yataongeza pato la uchumi kwa sababu yatavutia watalii kutoka nchi mbalimbali.

Aliwakumbusha Watanzania kuendelea kujikinga na vizuri vya ugonjwa wa corona ambao umekua ni tishio duniani.

Michezo

Ijumaa Juni 5, 2020

Nipashe



Muller auchambua uwezo wa Lewandoski

HABARI UK 22



Mshambuliaji wa Yanga, David Molinga (kulia), akimtoka beki wa timu hiyo, Ally Ally, katika mazoezi ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Bara yaliyofanyika kwenye uwanja wa Chuo cha Sheria jijini Dar es Salaam. **PICHA: YANGA**

# MAMBO MATAMU YASUBIRIWA YANGA

●●●Kocha wake Mbelgiji sasa kurejea nchini Jumapili, kujipima na KMC…

**Na Saada Akida**

HATIMAYE uongozi wa Yanga umetangaza Kocha wake Mkuu, Mbelgiji Luc Eymael, atarejea nchini Jumapili ili kuendelea kukinoa kikosi chake kinachojiandaa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na michuano ya Kombe la FA, imeelezwa.

Hata hivyo, hatima ya safari ya kocha wake wa viungo, Riedoh Berdien aliyeko Afrika Kusini haijajulikana kutokana na nchi hiyo kutofungua mipaka ya anga lake.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, alisema mchakato wa safari ya kocha wao umeshafanyiwa kazi kwa ajili ya kuja kuungana kuendelea na majukumu yake mapema.

Bumbuli alisema uongozi unasikitishia kumkosa kocha wake wa viungo, Berdien ambaye amekwama Afrika kusini lakini wanaamini kurejea kwa Eymael kutaongeza nguvu kwenye kikosi chao.

"Uhakika wa Luc kutua nchini sasa ni Juni 7, lakini suala la kocha wa viungo bado haijajulikana kwa sababu wenzetu Afrika Kusini bado mipaka yao imefungwa, hivyo tunasubiri tuone baada ya siku 14 walizopewa tena za 'lock down' itakuajе," alisema Bumbuli.

Kiongozi huyo alisema Yanga inaendelea kujiimarisha ili kupata matokeo mazuri katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zilizobakia na kufanya mchakato wa kusajili wachezaji wenye viwango vya juu kwa ajili ya msimu ujao.

"Siku ambayo kocha (Eymael), atatua nchini, kikosi chetu kitakuwa kinacheza mechi ya kujipima nguvu dhidi ya KMC FC kwenye Uwanja wa Uhuru, tunaamini mchezo huu utalisaidia benchi letu la ufundi kuangalia wapi kikosi kimefikia," Bumbuli alisema.

Aliongeza pia Yanga imepanga kuwachukulia hatua wachezaji wake ambao watabainika walikiuka maelekezo kutoka kwa makocha wao baada ya ripoti ya daktari wa klabu hiyo kuwasilishwa.

"Wachezaji wote ambao watabainika kwenda kinyume walipokuwa nyumbani wakati wa mapumziko ya corona watachukuliwa hatua, ripoti ya madaktari itakabidhiwa kwa benchi la ufundi, halafu hatua dhidi yao zitafuta," Bumbuli alisema.

Kwa sasa kikosi cha Yanga kinaendelea na mazoezi kwenye Uwanja wa Chuo cha Sheria jijini chini ya Kocha Msaidizi, Charles Mkwasa na Manyika Peter.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kurejea tena Juni 13, mwaka huu TFF na Yanga itakuwa ugenini kwenye Uwanja wa CCM, Kambarage mkoani Shinyanga kuwakabili wenyeji Mwadui FC.

Hadi Ligi Kuu inasimama Machi 17, mwaka huu, mabingwa watetezi Simba ndio walikuwa wanaongoza katika msimamo wakiwa na pointi zake 71, wakifuatiwa na Azam FC yenye pointi 54 baada ya timu zote kucheza mechi 28, wakati Yanga yenye pointi 51 ni watatu, lakini wana mechi moja mkononi.

Namungo FC ya Lindi inayoshiriki ligi hiyo kwa mara ya kwanza ina pointi 50 na iko kwenye nafasi ya nne na Coastl Union ya Tanga inakamilisha 'Tano Bora' ikiwa na pointi 46 wakati Singida United inashika mkia ikiwa na pointi 15.

## Simba hesabu zote kwa Ruvu

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema anahitaji kupata mechi ya kirafiki kwa ajili ya kujiweka imara na tayari kuwakabili Ruvu Shooting katika mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Juni 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Sven aliliambia gazeti hili kuwa mechi hiyo ya kirafiki itamsaidia kujua ubora wa kikosi chake ili kukamilisha malengo yake kabla ya kurejea katika mechi za ushindani.

Mbelgiji huyo alisema anahitaji kuona Simba inapata ushindi katika mechi zote za Ligi Kuu Bara zilizosalia, hivyo anahitaji 'kukipasha' kikosi chake baada ya kutoka kwenye likizo ndefu ya mapumziko ya corona.

"Nahitaji mechi ya kirafiki, ninaamini itanipa mwanga wa kuona ubora wa kikosi changu, lakini bado sijajua nitacheza na timu gani au siku ipi, bado nimeuachia uongozi suala hili," alisema Sven.

Aliongeza muda wa maandalizi wa wiki mbili ambao wameupata, kwake unatosha kukijenga na kukiweka kikosi chake tayari na mapambano ya lala salama.

"Kabla ya kupata mechi ya kirafiki, muda huu nitaendelea kubadili programu mbalimbali za mazoezi, kwa kadri tunavyozidi kwenda mambo yanabadilika, ninavutiwa na kasi yao, kila mmoja anaonekana yuko tayari kuendelea na mbio za ubingwa," alisema kocha huyo.

Vinara hao wa Ligi Kuu Bara watarejea kwenye kampeni ya kutetea taji wanalolishikilia la ligi hiyo kwa kuwakaribisha 'Maafande' wa Ruvu Shooting, Juni 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

Simba yenye pointi 71, na yenye michezo 10, inahitaji pointi 15 ili kufikisha pointi 86 ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine yoyote msimu huu.

Endapo itafanikiwa kutwaa ubingwa wa msimu huu, Wekundu wa Msimbazi watakuwa wamechukua taji hilo kwa mara ya tatu mfululizo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >